

# families worldwide

Nambari 25 Juzuu ya 1.20

Kujenga  
Matumaini  
na Hakika



# Mada 2020: 2020 Kujenga Tumaini na Imani

Wakati wa mchakato wetu wa kimataifa wa kusikilizana unaoitwa MULOA (Mothers' Union Listens, Observes and Acts – Ushirika wa Akina Mama Huzikiliza, Huchunguza na Huchukua Hatua) sauti za wanachama zaidi ya 200,000 kote duniani ziliweza kusikika.

Hii iliiwezesha Baraza la Dunia kuleta pamoja vipengele muhimu vinavyojitokezea na hivyo kuunda mwelekeo wetu sisi kama jumuia.

Mwito wa “Kujenga Tumaini na Imani” umewekuwa chachu ya wito wetu wa kuwasaidia watu binafsi na familia ili wabertilishie maisha yao. Huku tukiwa tunajenga matumaini yetu na imani kwa Mungu tutapata msukumo na ukakamavu wa kujenga matumaini na imani kwa watu wengine, hapa nchini kwetu na vilevile katika kiwango cha kimataifa.

Nyenzo na mwenendo wa mwaka 2020 unapatikana kwenye mtandao huu:

[www.mothersunion.org/2020-theme-building-hope-and-confidence](http://www.mothersunion.org/2020-theme-building-hope-and-confidence)

## YALIYOMO



- 4 Barua la Raisi wa kidunia
- 6-7 Ukanda wa A: Korea, Myanmar, India Kaskazini, India Kusini, Sri Lanka
- 8 Ukanda wa B: Kanada, Marekani Kusini, Marekani, West Indies
- 9 Ukanda wa C: Aotearoa, Nyuzilandi na Polynesia, Australia, Melanesia, Papua New Guinea
- 10-11 Ukanda wa D: Kenya, Uganda, Rwanda, Tanzania, Yerusalem na Mashariki ya Kati
- 12-13 Ukanda wa E: Afrika ya Kati, Nijeria, Sudan Kusini, Sudan, Kusini mwa Afrika
- 14 Ukanda wa F: Burundi, Kongo, Bahari ya Hindi, Afrika Magharibi
- 15 Ukanda wa G: Canterbury      **Ukanda wa H:** York
- 16 Ukanda wa I: Irelandi yote      **Ukanda wa J:** Scotland  
Ukanda wa K: Wales
- 17-46 Shajara ya Maombi:** Januari – Juni 2020
- 24-25 Ramani ya Wanachama**

*Families Worldwide* ni rasilimali ya kuongeza maarifa kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, inayochapishwa mara mbili kwa mwaka na kusambazwa bure kwa wanachama na marafiki walio Uingereza na Irelandi. Wanachama wa nchi za kigeni na marafiki wanawezza kupokea nakala ya PDF kupitia barua-pepe kuteka mikoa ya ndani. *Families Worldwide* sasa imetafsiriwa kwa lugha za Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili.

Andika barua kwa: Mothers' Union, Mary Sumner House, 24 Tufton Street, London, SW1P 3RB  
T: 020 7222 5533  
E: publications@mothersunion.org  
Registered Charity Number: 240531  
  
Rais wa kidunia: Sheran Harper  
Mkurugenzi mkuu: Bev Jullien  
*Families Worldwide* imechapwa na Mothers' Union

Mhariri kaimu: Beth Lanksford  
Msimamizi wa machapisho: David Baronti  
Kubuni: Arca Creative  
Kimechapwa na: Halcyon Print Management Ltd.

Karatsi iliyotumika katika chapisho hili imetengenezwa kwa kutumia mbao kutoka misitu endelevu na ambayo haina klorini. Huku kila juudhi ikiwa imechukulwa ili kuhakikisha usahili wa tarehe na maoni, Ushirika wa Akina Mama hauwezi kukubali jukumu kwa hasara yoyote, uharibitu au usumbufu unaosababishwa kwa makosa yoyote au upungufu.

© hati miliki ya yaliyomo 2019

**Dada na ndugu zangu wapendwa,**

Krisimasi ya mwaka huu ni ya kipekee kwa sababu tunasherehekea mambo mawili: Zawadi ya kuzaliwa kwa Yesu pamoja na sura mpya ya *Families Worldwide*. Kutokana na mazungumzo katika Baraza la Ulimwengu la mwaka wa 2019, gazeti hili sasa limetafsiriwa kwa lugha tatu: Kihispania cha Amerika ya kusini, Kiswahili na Kifaransa.

Haya ni mafanikio makubwa kwa vile wanachama zaidi kuliko hapo awali wataendelea kuunganishwa katika maeneo mbali na mbali kwa njia ya sala ya mchana. Kama mwanachama mmoja alivyoshuhudia, "Families Worldwide huandamana nami kila mahali. Kwa hivyo popote nilipo, mimi ni sehemu ya mzunguko wa maombi duniani kote." Hili ni jambo la kutia moyo kwa sababu wakati baadhi ya wanachama wanapumzika katika sehemu moja ya dunia, wengine wameamka na wanainua Ushirika wa Akina Mama katika maombi, kila dakika ya kila siku.

Mwelekeo mwingine mpya wa *Families Worldwide* ni kutengeneza upya maarifa ya maeneo badala ya kutumia maeleo mafupi ya nchi. Katika mwelekeo huu mpya maeleo muhimu ya athari na mabadiliko yameainishwa. Nina hakika kwamba mtawezwa kuufurahia mwelekeo huu kwa vile siwezi kufikiria njia bora zaidi ya kuonyesha kazi tunayofanya na familia na jamii, na wakati huo huo kuongeza uwezo wetu wa kufikia maeneo mbalimbali.

Huku tukifunga mikono yetu na kuukaribisha mwaka wa 2020, hebu tushikane mikono tuombe, tuulize mwongozo na mwelekeo wake Mungu katika mabadiliko tunayotamani kuyafanya na vilevile tuombe baraka zake hivi tunapoendelea kuwa waaminifu kwa utambulisho wetu sisi kama muungano.

**Bwana Mungu unayetupenda**

*Tunakushukuru kwamba Ushirika wa Akina Mama ni muungano wa kimataifa, unaoongozwa na wanawake kwa kujitolea kwao. Tunakushukuru kwamba tukiwa na umaja katika utofauti wetu na kuishi ndani ya imani yetu, sisi tunawapatia msaada watu binafsi na familia ili maisha yao yabadilike. Uwezo na neema zako zinatupatia nguvu ili tukae ndani ya Kanisa na jamii, ili tuweze kufikia watu kwa njia ambazo hazijonekana, ili tuweze kuwapatia sauti wanyonge na watu wanaoishi katika mazingira magumu. Tunakushukuru sana kwa baraka zako juu ya kazi yetu. Tunatokuza Jina lako Takatifu. Amina*

Ninawataki nyinyi pamoja na jamii zenu heri na baraka za mwaka mpya Pokeeni upendo na maombi yangu!

Sheran Harper  
Rais wa Ushirika Kimataifa



# Uanachama wa kidunia

Katika toleo hili la *Families Worldwide* tunwawashilishia nyanda 11 za Ushirika wa Akina Mama na mdhamini wao. Taarifa hizi kuhusu maeneo zimetayarishwa na wadhamini wa nyanda pamoja na Mary Sumner House, tena zinaweka pamoja namba za uanachama, taarifa kuhusu nyanda mbalimbali, miradi, mipango mipyä na hadithi za mabadiliko. Kama una ushuhuda ambao ungependa kushiriki katika eneo lako, tafadhalii tuljishe katika mtandao: communications@mothersunion.org, ili tuweze kuweka kipengele katika toleo lijao.

Kurasa za katikati za *Families Worldwide* (ukurasa wa 24-25) zina ramani ya mwanachama, inayodhihirisha ushirika wetu wa kimataifa wa wanachama duniani kote. Tumetumia uratibu wa rangi katika ramani hii ili uweze kuona ni nchi gani zilizo katika eneo fulani na pia idadi ya wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walio kwenye eneo hiyo. Ni matumaini yetu kwamba maarifa haya yatakutia moyo huku tukikiri vile tumeweza kufikia watu wengi kwa njia ya ajabu, sisi kama shirika ambalo ninyi mnasimamia sehemu kubwa.



Kwa mzunguko wa kisaa kutoka juu: Wanachama kusaidia wakati wa mafuriko katika Myanmar; ujumbe wa mwaka wa 2018 nje ya jengo la Umoja wa Mataifa, wanachama katika Lincoln, kuongeza ufahamu wa unyanyasaji wa kijinsia, Wanachama katika Tampa Bay, Florida, Kikundi cha kuweka hazina na kukopa nchini Rwanda.



## Korea, Myanmar, India Kaskazini, India Kusini, Sri Lanka

**Mdhamini:** Roshini Mendis

**Idadi ya Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 1,915,369

**Lugha kuu:** Kihindi, Kiberma, Kikorea na KiSinhali



**Ukanda wa A unashughulikia nchi zetu za bara la Asia na unashirikisha idadi kubwa zaidi ya wanachama wa Ushirika wa Akina Mama ambao ni zaidi ya milioni 1.9! Idadi kubwa ya hawa ni wanachama wa Women's Fellowship for Christian Service (WFCS) kutoka Kaskazini na Kusini mwa India. Ukanda huu una jumla ya wakazi bilioni 1.4 hivi kuufanya mkubwa zaidi katika suala la wakazi na uwezo wa kuwafikia.**

Baada ya kumaliza MULOA, wanachama katika Ukanda wa A walikubaliana kuwa maombi yanapaswa kuwa lengo kuu katika yote ambayo wanayofanya. Kama kanda zingine, waliweza kutambua baadhi ya watu waliohitaji msaada, nao ni watoto wasiojiweza, wanawake walio pembeni ya maendeleo na watu wanaoishi kwa hali ya upweke. Waliamua kufanya hivyo kwa njia mbalimbali. Kwa watoto wasiojiweza wanachama walilenga kuboresha lishe

na afya zao na kusaidia katika kupata elimu. Nchini Sri Lanka, tayari wanasaidai kusomesha lugha ya Kisinhali, Kiingereza na hesabu bila malipo. Wanaleta chai na vinywaji kwa ajili ya wagonjwa na wageni katika kitengo cha magonjwa ya moyo cha hospitali kuu ya taifa na katika Hospitali ya Watoto ya Kitaifa nchini Sri Lanka. Mradi mmoja mahususi unaitwa "Christ Care" ambapo mara moja kwa wiki, familia zinaweza kuleta watoto wao walemaru kwenye ukumbi wa kanisa ambapo wanachama hutoa tiba ya mwili, elimu maalum na chakula. Wakati huo huo, wazazi wa kike wa watoto hao wanafundishwa jinsi ya kushona foronya na njia za kuwatunza watoto wao. Watoto kumi na watatu wa dini mbalimbali - Ukristo, Uislamu, Uhindu na Ubuddha - sasa hivi wanahudhuria mpango huu.

Kwa wanawake walio pembeni mwa maendeleo, wanachama walitaka kuongeza maarifa kuhusu ukosefu wa usawa wa kijinsia. Huko Myanmar wanafanya hivyo kwa kujihusisha na wanaume na kushirikiana pamoja na Bread for the World na Diakonia.

Hatimaye, ili waweze kuwasaidia watu walio katika hali ya upweke, wanachama waliamua kulipa kipaumbele jambo la kuwatolea huduma, kuwatemeblea na kuwasaidia wale ambao hawana mwingine yeyote wa kuwasaidia maishani mwao. Katika Sri Lanka wanachama hujitolea



Wanachama wa Myanmar katika warsha wa Asia MULOA 2

kwenye makazi ya wazee kwa kuwapatia upendo na huduma. Huko Korea ya Kusini wanaendesha miradi ambayo husaidia watu walio katika hali ya upweke. Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama hutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya makuhanu wastaaful ambaao ni wagonjwa. Wanasaidai watu ambao hawana makazi, na vilevile kuwapa msaada wagonjwa wa Alzheimer.

Nchini Myanmar, familia 385 zimesaidiwa na Ushirika wa Akina Mama katika mpango wa mikopo midogo. Mpango huu umetoa

msaada wa kiufundi kwa wale ambao wamejajiri na mikopo kutolewa kwa ajili ya wale ambao wanaihitaji.

Kupitia mradi wa MULOA, baadhi ya mambo yamepewa kipaumbele hasa yanayohusiana na utetezi na sera ya mabadiliko yalio dhahiri. Mambo hayo ni kama biashara ya kuza binadamu nchini India na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) katika Myanmar. Katika maeneo haya yote wanachama wanataka kuongeza utambulizi wa masuala ili kupunguza kiasi cha waathiriwa na kubadilisha sheria ya ulinzi.

### Hadithi za mabadiliko

Nchini Sri Lanka wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walijitolea kusaidia mama moja ambaye mtoto wake ni mlemapu. Alikuwa akienda hospitalini mara nyingi kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha mikono na miguu kwa viungo bandia. Hivi sasa yeeye anaweza kutembea, anahudhuria shule na anafanya vizuri katika masomo yake.

Mtoto ambaye baba yake anatumikia

hukumu ya kifungo cha maisha Familia yake inashukuru Ushirika wa Akina Mama kwa sababu bila msaada wao, angekuwa ameacha shule kutokana na ukosefu wa fedha.

Watoto hawa wote wawili walisaidiwa baada ya wanachama kumaliza MULOA iliyowaonyesha kwamba ni lazima kusikiliza kilio cha wenye mahitaji.

## Kanada, Marekani ya Kusini, Marekani, West Indies

**Mdhamini:** Kathleen Snow

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 13,271

**Lugha kuu:** Kingereza, Kifaransa, Kihispania, Wichi, Toba, Kiholanzi, Papiament



Nchi za Ukanda wa B zikijumuishwa kwa pamoja, idadi ya wakazi inafiki karibu bilioni moja. Kwa upande wa ukubwa wa kijografia hili ndilo eneo letu kubwa zaidi likiwa na 42.5km<sup>2</sup>. Ukanda wa B ulikuwa eneo la kwanza kwa majaribio ya MULOA hapo mwezi wa Septemba mwaka wa 2017 ambapo takribani wanachama 6,000 walikuwa wameonyesha shauku katika kushiriki kwa mchakato. Waligundua kwamba mandhari sawa na hizi zilikuwa zinatokezea katika sehemu mbalimbali. Tena, wanachama waliazimia kuwafikia watu wanaoishi katika mazingira magumu na haliduni, vilevile kuwafikia na kutetea watu walionyanyaswa na kukosa haki zao.

Uzazi wa mpango umefaulu sana katika eneo hili na hivi sasa unaendelea katika nchi za Kanada, Argentina, Guyana na West Indies. Zaidi ya watu 15,000 tayari wamesaidiwa na kuna mipango ya kuanzisha miradi huko Marekani, na vilevile kwa wakazi wa kiasili wanaojulikana kama Cree huko Kanada.



Washiriki huko Merika huandaa chakula kwa mtu kofia na kuu.

Kutambua biashara ya uuzaji wa binadamu kumepewa kipaumbele nchini Kanada, Marekani na West Indies, kama vilevile harakati juu ya madawa ya kulevyia na uhalifu katika Amerika ya Kusini.

### Shuhuda za mabadiliko

Wanachama wa nchi ya Guyana wamekuwa wakitengeneza vifaa vya kujihifadhi wakati wa siku zao ili waweze kuendelea kuhudhuria shule. Na katika Argentina kaskazini, wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walijunga na Kanisa la Katoliki katika maandamano dhidi ya dawa za kulevyia huko mjini Juarez.

Wanachama wa tawi moja katika Marekani walikuwa wakifanya kazi pamoja na wakimbizi kutoka Afrika na badala ya kuwapa zawadi wakati wa Krismasi, waliwaliza wataje vitu walivyohitaji. Sasa wanachama wameanzisha soko la kupeana chakula kwa ajili ya watoto huko wakitoa msaada nyakati za dharula.

## Aotearoa, Nyuzilandi na Polynesia, Australia, Melanesia, Papua New Guinea

**Mdhamini:** Libbie Crossman

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 45,323

**Lugha kuu:** Kingereza, Kimaori, Solomon Island Pidgin, PNG Pidgin, Motu + Zaidi ya lugha za kiasili 700 zavisiwani



waweze kusaidiwa na kushikwa mkono. Hatimaye, katika Melanesia na Papua New Guinea - wanachama wangependa kuona ushirikishwaji zaidi wa watu walemvu katika jamii.

Mpango wa malezi bora nchini Melanesia umefanikiwa sana na tayari umesaidia watu binafsi 2000. Wanachama wameona upungufu wa vurugu ndani ya familia na vilevile baina ya familia mbalimbali. Mipango ya ufundishaji wa kusoma na kuandika katika Melanesia na Papua New Guinea imesaidia watu zaidi ya 8,000 na wanachama wameweza kuhamasisha elimu ya watoto - hasa wasichana.

### Hadithi za mabadiliko

Tawi moja nchini Australia sasa hupeana chakula ya kifungua kinywa kwa ajili ya watoto ambao husafiri masafa marefu kwenda shulen. Makanisa mengine katika mji huo walitoa msaada na wakashinda kikombe kinachotolewa na serikali ya Jimbo kwa ajili ya huduma kwa jamii. Sasa, matawi mengine ya Ushirika wa Akina Mama nchini kote wanaanzisha mipango kama hio.

Mpango wa ulezi katika Melanesia unarejesha uhusiano. Katika tukio moja, kijana mmoja alirudi nyumbani baada ya miaka miwili ya kukataa kuijunga na familia yake.

## Kenya, Uganda, Rwanda, Tanzania, Yerusalem na Mashariki ya Kati

**Mdhamini:** Mary Kamwati

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 1,019,591

**Lugha kuu:** Kinyarwanda, Kingereza, Kiswahili, Luganda, Kiarabu, Kiyahudi



**U**kanda huu unashirikisha hasa nchi za Afrika mashariki pamoja na Yerusalem na nchi katika Mashariki ya Kati (ambazo ni pamoja na Jimbo la Saiprasi). Watu milioni 573 wanaishi katika eneo hili, wengi wao wakiwa wanaishi katika Mashariki ya Kati. Tanzania ndiyo inachukuwa nafasi ya pili kwa ukubwa wa idadi ya wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, wakiwa zaidi ya 850,000!

Kupitia mchakato wa MULOA, wanachama katika Ukanda wa D walisema kwamba 'sala' ilikuwa mada kuu iliyojitokeza. Walikubaliana kwamba makundi matatu ya kwanza ya watu walio taka kuwfikia na kuwapatia msaada ni walemvu, wafanya biashara ya ngono na watu wanaoteseka na VVU / UKIMWI. Walikubaliana kwamba

kwanza walihitaji kusikiliza zaidi na kisha kujenga mazingira salama kwa ajili ya watu walio taka kusaidia. Walitambua kwamba kujenga mitando na wanachama wengine na mashirika kutafa idisha kazi zao. Tena, kuhamasisha na kuwaandalia watu vifaa katika jamii zao ili waweze kutambua na kutumia rasilimali zao ndilo jambo litakaloleta mabadiliko bora zaidi.

Nchini Kenya, Rwanda, Uganda na Tanzania, mawanda makuu yaliopewa kipaumbele cha mabadiliko ya sera na utetezi ni kampeni dhidi ya ukeketaji (FGM) na ndoa za utoton - huku mabadiliko yanayotakikana yakiwa "kikomo kamili" cha mazoea haya. Idadi kamili haijulikani lakini wanachama tayari wanaleta mabadiliko katika mitazamo ya ukeketaji ndani ya jumuia ambazo zina desturi hii. Nchini Kenya, wanachama wanatoa changamoto ndoa ya utoton na wakati mwингine wamekuwa na uwezo wa kuzizua. Mara nyiningi imebidi wanachama wapeleke wasichana walio hatarini katika maeneo salama ili kuwalinda kuto kana na ndoa kabla hawajatimiza umri wa kuolewa.

Upungufu wa unyanyasaji na mashambulio ya kijinsia ni jambo mashambulio ya kijinsia ni jambo liliopewa kipaumbele nchini Rwanda kipaumbele nchini Rwanda. Pia kuna hamu ya kuwezesha watoto wote kupata elimu nchini Kenya. Wanachama wanataka kuona mabadiliko katika sheria



Kikundi cha mradi wa mikopo katika Gisanga, Rwanda

ili wazazi ambao hawapeleki watoto wao shulen waadhibiwe.

Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama wanashiriki katika miradi na mipango mingi katika eneo hili. Nchini Uganda, wanachama hufundisha wasichana kutengeneza sodo. Tena wao wanasi mamia kantini ya shule, wanapanda miti na kuendesha vituo vya huduma za elimu kwa watoto wachanga. Nchini Kenya wao wana mpango wa chakula mashulen, kundi la ushirika kwa wajane na tena wao huendesha mipango ya ulezi na utoaji wa mashauri kwa vijana. Huko Rwanda na Tanzania, wanachama wote wana endesha mipango ya akiba na mikopo ambayo imefanikiwa sana. Huko Tanzania wanatia njiani semina na warsha kuhusu maisha ya familia, huduma na afya ya watoto.

Katika Mashariki ya Kati tuna wanachama nchini Iraki, Saiprasi na Misri. Ingawa 1% tu ya idadi ya watu katika Iraki ni Wakristo, wanachama wa Ushirika wa Akina Mama nchini hiyo wanajitolea sana katika kazi kwa jamii zao. Kuna hisia

kali ya kiroho na ushirika kati yao. Hafla maalum kama vile Jumapili ya uzazi, Krismasi na Pasaka zinasherehe kewa kwa nyimbo, sifa na shangwe nydingi. Kazi yao ya vitendo vya kuwfikia watu zinakadiriwa na familia kwa sababu hakuna huduma au msaada rasmi nchini Iraki, kwa ajili ya watu wanaoishi katika mazingira magumu. Baadhi ya kazi wanayofanya ni pamoja na mipango ya chakula, huduma kwa yatima, kutembelea wagonjwa na shule ya Jumapili.

### Hadithi za mabadiliko

Una madre y su hija fueron expulsadas de su familia por el padre. La madre se hizo miembro de la Unión de Madres y la ayudaron a reconciliarse con su esposo y a acceder a la educación.

Una mujer escuchó acerca del amor de Mary Sumner y sintió el deseo de actuar como ella actuó. Cuando su suegra enfermó de tal manera que ya no podía ir a la iglesia, ella y su esposo compraron un vehículo para poder llevarla.

## Afrika ya Kati, Nijeria, Sudan Kusini, Sudan, Kusini mwa Afrika

Mdhamini: Thembsie Mchunu

Wanachama wa Ushirika Wa Akina Mama: 259,168

Lugha Kuu: Kiingereza, Nguni, Kireno, Dinka, Kiarabu, Shona, Yoruba, Abon



**U**kanda wa E una idadi ya watu milioni 419 na unashirikisha nchi 15 za Afrika zilizo na wanachama wa Ushirika Wa Akina Mama. Zaidi ya wanachama 100,000 walishiriki katika mchakato wa MULOA - zaidi kuliko maeneo mengine!

Wanachama 170 kutoka Sudan Kusini walishiriki katika warsha ya wiki mbili ya MULOA ilioandalishi na dayosisi ya Madi West Nile kaskazini mwa Uganda hapo mwezi wa Februari 2019. Semina hii iliwapatia washiriki nafasi ya kutafakari juu ya ushiriki wao katika Ushirika Wa Akina Mama na vilevile juu ya hali katika nchi yao wenyewe. Wanachama wengi walisafiri hadi kambi za wakimbizi kaskazini mwa Uganda kutembelea jamaa amba wengine hawakua wameonana kwa muda wa miaka mingi. Baadhi ya jamaa hawa ni pamoja na watoto wao.

Kama kanda zingine, kwa njia ya kushiriki katika MULOA, wanachama wa ukanda wa E walikubaliana kuwa walitaka kuzingatia msaada wao kwa watu wanaoishi katika mazingira duni, wale wasiojiweza na wale walioathiriwa na umaskini. Walitaka kufanya hivyo kwa njia ya kuishi katika imani, utetezi, elimu, na kuhusisha watu kwa huduma za serikali. Pia walihitimisha kuwa ujenzi wa kujitegemea na mazingira yenye usalama kwa ajili ya watu waliotaka kuwafikia ungeweza kuwasaidia kubadili maisha yao wenyewe.

Kusini mwa Afrika maeneo ya kipaumbele kwa utetezi na sera ni kubadilisha mawazo kuhusu ulemavu wa ngozi na VVU / UKIMWI na vilevile kuingiza watu hawa zaidi ndani ya mfumo wa jamii kwa njia ya kuelimisha jamii. Wanachama kusini mwa Afrika pia wanataka kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Katika Sudan Kusini na Kati aula za kwanza kuhusu mabadiliko ni kukomesha ndoa za kulazimishwa pamoja na unyanyasaji wa kijinsia (GBV).

Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama katika eneo la kati na kusini mwa Afrika tayari wamekuwa wakiongeza ufahamu kuhusu ukatili wa kijinsia. Jambo la kushangaza ni kwamba takriban watu 60,000 wamesaidiwa hadi sasa, huku wanaume wakijiunga kwa kampeni iitwayo 'Si kwa jina langu' na kuahidi kulinda wanawake.



Miembros de Sudán del Sur celebrando grupos familiares como parte de MULOA.

Katika ukanda mzima kumekuwa na washiriki 12,000 katika vikundi nya Mikopo, Akiba na Ufundishaji wa kusoma na kuandika. Kutokana na hayo wanawake wamepata uhuru zaidi na hatimaye kuwa na uwezo wa kujengewa nyumba kwa ajili ya familia zao. Mchakato wa Uhamasishaji Kanisani na katika Jamii (CCM) umebadilisha maisha ya watu 40,000 walio na mawazo mabaya huku watu binafsi wakipata nafasi ya kujifunza kujifanyia mambo yao wenyewe.

Ingawa Sudan ndiyo nchi ya tatu kwa ukubwa katika Afrika, Wakristo katika nchi hii ni wachache sana wakiwa 1% tu ya idadi ya watu nchini. Kwa hiyo, ikilinganishwa na maeneo mengine ya ukanda, uanachama wa Ushirika wa Akina Mama nchini Sudan ni mdogo wakiwa watu 400 pekee. Lakini unaendelea kukua kwa kasi kila mwaka. Wanachama ni wachangamfu sana katika jamii zao, wakiwa wanawahudumia watu wote bila kujali jinsia, umri, dini au kabilu. Miradi yao ni pamoja na kutembelea wagonjwa katika hospitali, kuhubiri gerezani, kutoa mafunzo ya ufundi, amani na maridhiano, mpango wa elimu ya kibiashara pamoja na kujifunza kusoma na

kuandika. Wanachama huwa wanahudhuria mikutano ya kila mwezi ya Ushirika wa Akina Mama. Sala ni muhimu kwa kila wanachokifanya.

### Hadithi za mabadiliko

Kikundi cha wanachama wa Ushirika wa Akina Mama katika ukanda huu wamesaidia shule moja ilio katika mahitaji. Walianza kwa kununulia watoto sare na vifaa nya shule. Tena, baada ya MULOA, walianza kusikiliza wazazi wa wanafunzi ili kugundua ni vitu gani hasa walivyohitaji. Baadhi ya familia sasa zimeunganishwa na idara za serikali zinazohusika na wakawea kupokea misaada.

Wanachama nchini Zimbabwe wamekuwa wakifanya kazi na kundi la wauguzi kutoka Hospitali ya Bonda Mission katika kuwafikia wakazi walio na mahitaji yanayohusiana na afya. Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama husafirisha wauguzi kwenda maeneo ya vijijini ili waweze kuwahudumia wagonjwa wa saratani, ugonjwa wa kisukari au msukumo wa damu.

## Burundi, Kongo, Bahari ya Hindi, Afrika Magharibi

**Mdhamini:** Marie-Pierrette Bezara

**Wanachama wa Ushirika Wa Akina Mama:** 56,599

**Lugha kuu:** Kifaransa, Kirundi, Kiingereza, Malagasi, Creole, Lingala, Kiswahili



**N**chi za Ukanda wa F zote kwa pamoja zina idadi ya watu milioni 204. Wengi wa watu wanaoishi huko huzungumza Kifaransa na Kiingereza. Wanachama katika eneo hili wanataka kusaidia familia, wanawake na wasichana hasa wale walio hatarini. Mandhari kuu ambazo zilijitekeza katika MULOA zilikuwa, afya na urejeshaji wa uhusiano, amani na usalama, na kulinda mazingira (kipaumbele cha kipekee nchini Madagaska). Wanachama wanataka kuhamasisha na kuandaa jamii zao kwa kujitegemea. Manda hizi zimekuwa sehemu ya mkakati wetu kwa ajili ya Ushirika wa Akina Mama duniani.

Kipaumbele cha mabadiliko ya sera na utetezi ni kupunguza unyanyasaji wa kijinsia katika eneo (hii inahusishisha unyanyasaji wa majumbani, unyanyasaji wa kijinsia na ukeketaji). Ulinzi wa mazingira kwa njia ya Maafa ya Kupunguza Hatari katika jimbo la Bahari ya Hindi, pamoja na haki za ardhi na raia kuhusu wajane katika Afrika Magharibi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) - wanachama wangependa wajane wapate uwezo wa kuhifadhi mali yao bila kulazimishwa kuolewa tena.

### Shuhuda za mabadiliko

Katika Dayosisi ya Toamasina, Madagaska, wanachama wa Ushirika wa Akina Mama wakishirikiana na wabia wengine wamesaidia wanawake wanaoishi na ugonjwa wa fistula. Kwa kawaida wanawake hawa walikuwa wanatengwa na jamii zao na waume wao. Kwa hivyo walikuwa na aibu ya ugonjwa wao, na kujihisi kama wamekataliwa.

Matokeo yake, wanawake na familia zao walikosa kujitegemea kifedha. Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walianzisha miradi iliyosaidia wanawake kurejesha hali ya kujiamini kwao. Walifundishwa ujuzi mpya na masomo kutokana na Biblia na wakaanza kuamini Mungu tena na kuelewa zaidi kuhusu maradhi yao.

## Canterbury

**Mdhamini:** Nikki Sweatman

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 26,900

**Lugha kuu:** Kiingereza



**M**koa wa Canterbury ni moja ya dayosisi katika Ulaya ambapo kuna zaidi ya wanachama 200 wa Ushirika wa Akina Mama, wakiwa nchini za Ubelgiji, Saiprasi, Denmaki, Ufini, Ufaransa, Ujeruman, Italia, Malta na Gozo, Uholanzi, Ureno (ikiwa ni pamoja na Madeira), Uhispania (ikiwa ni pamoja na Visiwa vya Kanari), na Uswisi. Wanachama katika eneo hili wanashiriki katika aina mbalimbali za miradi na moja ya kipaumbele kinachotiliwa mkazo ni utumwa wa siku za kisasa. Wanachama wanataka kuongeza ufahamu na kujihusisha na mashirika, na Kanisa kuu ili kupunguza idadi ya watu wanaokabiliwa.

### Shuhuda za mabadiliko

Kiingereza kwa Wanawake (English for Women) ni mradi katika eneo hili ambao husaidia wanawake 120 na watoto 40 wa mataifa 20 tofauti kwa kuwafundisha na kuwaingiza katika utamaduni wa Kiingereza. Hii imezuiya kutengwa, tena imesaidia mawasiliano na mpango huu unaigwa katika maeneo mengine ndani ya Mkoa wa Canterbury.

## York

**Mdhamini:** Catherine Hilton

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 18,025

**Lugha kuu:** Kiingereza



**K**una watu milioni 16 wanaoishi katika Mkoa wa York, na watu 273,400 kati yao ni Waanglikana. Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama husaidia watu walio hatarini, wale wanaokabiliwa na mashaka na upweke. Wao hufanya hivyo kwa kutoa huduma ya uchungaji na huduma za dharura kwa wakimbizi, wazee, wafungwa, na wagonjwa katika hospitali. Mwezi wa Novemba mwaka wa 2018 tawi jipya lilifunguliwa wakati vijana wawili waliomba kuijunga na Ushirika wa Akina Mama. Wao wanajiita 'Mini MU' na sasa wapo zaidi ya wanachama vijana 20 wanaohuduria wakisaidiwa na wanachama watu wazima.

### Shuhuda za mabadiliko

Katika Jimbo la York familia ya wakimbizi wanane walipewa udhamini wa pamoja kutoka Ushirika wa Akina Mama na Home Office. Walipewa nyumba, vifaa, nafasi katika shule na sare za shule. Matibabu yaliandaliwa. Wanachama pia walisaidia kuandaa madarasa ya ESOL (Kiingereza kwa wanaoongea lugha nyingine) kwa ajili ya familia ili waweze kupata manufaa kutoka kwa Serikali.

## Irelandi Yote

**Mdhamini:** June Butler

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 7,000

**Lugha kuu:** Kiingereza, Kiairishi



Irelandi ina idadi ya watu milioni 6.7, watu 375,400 mionganii mwao wakiwa waabudu wa kanisa la Anglicana. Neno "Ireland Yote" linahusu maeneo mawili-Jamhuri ya Irelandi (ROI) na Irelandi ya Kaskazini ambayo iko chini ya utawala wa Uingereza. Ukanda huu una dayosisi 12 na wanachama hutumia wakati na rasilimali zao hususani katika kuongeza maarifa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, kutoa bidhaa na usaidizi kwa ajili ya wanawake walio katika ukimbizi. Wanasaadia watu kupata likizo, wanaendesha miradi katika magereza, na kusaidia jamii za parokia na wale walio wapweke, wale ambaa hawawezi kutoka majumbani mwao, au wale walio na ugonjwa wa dementia. Dayosisi ya Clogher iliandaa siku ya furaha ya familia, ambayo ilihudhuriwa na zaidi ya watu wazima na watoto 500. Kila mwaka, inatoa mahali pa kubadilishia watoto nguo na pa kuchezea wakati wa Mashindano ya Taifa ya Kulima katika ROI.

## UKANDA WA J

## Scotlandi

**Mdhamini:** Paul Hindle

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 497

**Lugha Kuu:** Kiingereza, Kigaeliki



Kuna watu 5,400,000 katika Scotlandi na 31,656 ni waabudu wa kanisa la Anglicana. Washiriki wa nchi ya Scotlandi hushonea watoto njiti na wale waliozaliwa wafu mavazi Pia wao wanahuisha wagonjwa wa Alzheimer katika kufuma, mradi ambaa huunganisha na kusaidia watu wengi tofauti kwa njia tofauti. Washiriki pia hujitolea katika nyumba za utunzi kwa kuendesha vikao vya kuimba kwa ajili ya wakaazi walio na ugonjwa wa dementia. Nyimbo hizi huwa ni zile walizozimba miaka ya awali, na vikao hivi vinafurahisha wote wanaohusika.

## UKANDA WA K

## Wales

**Mdhamini:** Jenny Barton

**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 5,665

**Lugha Kuu:** Kiingereza, Kiwelshi



Wales ina wakazi milioni 3.2 na idadi ya Kanisa ya 210,000. Kuna parokia 900 na Ushirika wa Akina Mama unawakilishiwa kwa 30% ya parokia hizi. Mfano mmoja wa kazi inayoendelea katika dayosisi ya Llandaff ni ushirikiano pamoja na makazi ya Gwalia ambapo wanachama huchangia chakula na vifaa vya mwanzo kwa vijana wasio na makazi, ambao baadhi yao wana matatizo ya afya ya akili. Washiriki wa Ushirika wa Akina Mama pia wamekuwa wakiwafunza ujuzi mpya kama vile kupika, kujenga kujithamini kwao na ujasiri ili kuwatayarisha kwa maisha ya kujitegemea.

# Sala la kujiunga

Jiunge na wanachama wenzako wa Ushirika wa Akina Mama kote duniani huku tukiweka familia na miradi duniani kote katika maombi yetu

Maombi ni muhimu kwa kazi yetu kama Ushirika wa Akina Mama na kila siku, saa sita za mchana, wanachama duniani kote wanachukua muda wa kuomba. Wimbi la Maombi ni dhihirisho endelevu la kujitolea kwetu katika kuombeana sisi kwa sisi, ambalo linaendelea mwaka mzima na linashirikisha maeneo yote ambapo tumewakilishwa.

Unaweza kutumia maombi haya kila siku, kila wakati ili ujiunge na hili Wimbi la Maombi kote duniani, linaloyaombea majimbo kwa duru. Kalenda imegawanywa katika sehemu za siku tatu wakati sisi huomba kwa ajili ya kundi la majimbo. Siku moja ya wiki kuna aya ya Biblia ambayo unaweza kutafakari juu yake na kuchukua nafasi ya kuombea masuala ya kazi ya Ushirika wa Akina mama duniani kote unayoyafikiria wakati huo.

Huku sisi tukichukua jukumu letu la kuendeleza Wimbi la Maombi, tunaweza kufanya hivyo kwa kujiamini, tukijua ya kwamba maombi yetu yana maana na nguvu. Tunajitia moyo tukijua ya kwamba duniani kote kuna wengine ambaa, kwa njia hiyo hiyo wanatuombea. Na sasa kwamba *Families Worldwide* imetasiriwa katika Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili ni rahisi zaidi kwetu sisi kuomba kwa ajili ya kila mmoja.

Yesu, Bwana wa uhai wetu, kwa nguvu ya neno lako na kwa njia ya matendo yako ya upendo, tuite kuwa wanafunzi wako. Tupe nguvu ya kuwa tofauti, kusimamia haki na amani na kuwa na dalili za upendo wako unaopatanisha watu wote.

Mungu wa neema, utuwezeshe sisi watumishi wako kufanya lengo lako duniani kupitia kwa kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Leo tunaomba kwa ajili ya : \* tazama Shajara ya Wimbi la Maombi.

Tunawaombea wanachama wote.

Mungu awe pamoa nao katika kila sehemu zote za maisha yao, awahimize na awaongoze, awahifadhi na awape nguvu ili waweze kufanya kazi ya kukuletea sifa na utukufu. Amina



**Twamshukuru  
Mungu siku  
zote kwa ajili  
yenu nyote,  
tukiwataja  
katika maombi  
yetu.**

**1 Wathesalonike  
1:2**

## Jumatano 1

Imani kamwe hajui pahali inapoongozwa, lakini inampenda na inamjua Yule ambaye ni kiongozi wake *Oswald Chambers, 1874-1917, Mwinjilisti na mwalimu kutoka Scotland*. Bwana Mungu katika siku hii ya kwanza ya mwaka huu mpya sisi tunaweka imani yetu kwako wewe kwa yote yaliyo mbele yetu.

## Alhamisi 2

Tunaleta maombi yetu leo kwa ajili ya wanachama wote wa Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Waingie katika mwaka ujao kwa furaha na imani katika Bwana wetu, ambaye anashikilia maisha yetu ya baadaye kwa mikono yake.

## Ijumaa 3

Bwana utupendaye, imani yetu ipo kwako: tuna Imani kwa mipango yako ya baadaye ambapo sisi tutazaa matunda ya milele huku sisi tukiifuata amri yako. Siku zote tuwe chanzo cha baraka kwa dunia ambayo umetuita kuitumika.

## Jumamosi 4

"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho". *Yeremiah 29:11*

## Wimbi la Maombi

**Januari 1-3:** Wadhamini na wafanya kazi wa Ushirika wa Akina Mama kote ulimwenguni

## Jumapili 5

Katika kina cha roho zetu, ipo pahali ambapo Mungu anaweza kuzungumza na sisi. Hebu tutumie muda katika nafasi hii ili tuweze kutambua mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu.

## Jumatatu 6 Epifania /sikukuu ya Majusi

Leo tunasherehekea ziara ya Majusi, ambao waliongozwa kusafiri ili wapate Familia Takatifu. Kama wao walitenda kwa hekima na busara, wao walishuhudia utimilifu wa maandiko huku Mungu akiwafunulia Yesu kuwa Masihi. Mungu atusaidie, kama wao, kutambua jukumu letu maishani.

## Jumanne 7

Tunaomba utambuzi kwa wanachama wetu huku wakihusika katika mipango ya familia na jamii zao. Tunaomba ili waongozwe na hekima ya Mungu ambaye huwapa kwa ukarimu wote waombao kwa imani.

## Jumatano 8

Bwana wetu, tusaidie kutambua ni nini tunafaa tuache kufanya na ni nini tunafaa tuanze kuchunguza.. ili tufanikiwe katika kusambaza upendo wako na kutimiza mapenzi yako kwetu. Amina

## Alhamisi 9

Njia zako ni kamili, Bwana nisaidie siku zote kutambua njia ambayo umenitayarishia na kufuata nyayo zako huku tukisafari pamoja.

## Ijumaa 10

Baba ulije mbinguni, asante kwa uongozi wako maishani mwangu. Nisaidie kuchukua wakati wa kutua na kusikiliza uongozi wako. Nikumbushe kila siku kuwacha roho yangu ikulenge wewe, ili kila kitendo ninachokifanya kiwe kimetokana na wewe.

## Jumamosi 11

Wala msiifuatishé namna ya dunia hii; mbali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. *Warumi 12: 2*

## Wimbi la Maombi

**Januari: 5-7** Eswatini; Ruaha, Tanzania; Aguata na Lagos Bara, Nijeria; Norwich, Uingereza; na Chotanagpur, India

**Januari 8-10:** Lesutu; Kibungo, Rwanda; Etche na Ogbomoso, Nijeria; Leeds, Uingereza na Hanuato, Visiwa vya Solomon

## Wito wa Ushirika wa Akina Mama Januari 12-18 2020

### Jumapili 12

Bwana wa mavuno, tunaomba tupate ukuaji katika uanachama wetu, kwamba dhamira yetu ya kutoa huduma ya Kikristo kwa familia na jamii itashamiri duniani kote.

### Jumatatu 13

Bwana utupendaye, tunaomba kwamba utupe nguvu tunapotafuta kushiriki upendo wako kwa njia ya kampeni yetu kwa haki za kijamii. Sauti ya Ushirika wa Akina Mama iheshimiwe na wote wanaoisikia.

### Jumanne 14

Tunaombea kazi ya Ushirika wa Akina Mama katika jamii zetu za mitaa, miradi yote na mipango inayofanywa na wanachama wetu huku wakionyesha upendo wa Mungu kwa njia ya maisha yao ya hatua aminifu.

### Jumatano 15

Bwana, tunakupa shukrani leo kwa dhamira ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote ya kuleta mabadiliko kwa watu binafsi, familia na jamii kwa njia za upendo, huruma, ujasiri na mashirika yasiyo ya hukumu.

### Alhamisi 16

Baba uliye mbinguni, tunakushukuru kwa wanachama kote ulimwenguni ambao wanatekeleza kwa uaminifu utume wa Ushirika wa Akina Mama, mara nyingi katika hali changamoto. Tafadhalii utubariki sisi wote huku tukijitahidi kukupenda pamoja na majirani wetu, kwa moyo wetu wote.

### Ijumaa 17

Bwana, tunakushukuru kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama ambao, kwa miaka mingi, wametumia vipawa ambavyo umewapa ili kubadilisha dunia. Tusaidie kugundua uwezo wako ndani yetu, na njia ambazo tunaweza kuutumia kwa utukufu wako.

### Jumamosi 18

Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote; na jirani yako kama wewe mwenywewe. Luka 10:2

#### Wimbi la Maombi

**Januari 12-14:** Morisi; Kericho, Kenya; Katsina, Nijeria; Kumasi, Ghana; Winchester, Uingereza na Nandyal, India

**Januari 15-17:** Ushelisheli; Bokodi, Uganda; Enugu, Nijeria; Birmingham, Uingerezana; Marathwada, India

## Umoja wa Wakristo

## Januari 19-25 2020

### Jumapili 19

Yesu aliwaombea wanafunzi wake kwamba 'wawe na umoja ili ulimwengu upate kuaminini' Yohana 17:21. Kote duniani miyo inaguswa kama Wakristo wanaungana kuombea umoja. Bwana, siku ya leo ambayo sisi tunakusanyika kuabudu, tunatangaza umoja wetu katika Kristo.

### Jumatatu 20

Bwana utupendaye, tunakushukuru kwa furaha ya kuwa jamii katika Kristo na wanachama wenzetu wa Ushirika wa Akina Mama, vile tukiunganishwa pamoja kwa maombi na ibada, tunafikia watu kwa upendo na huduma tukiwa mikono yako duniani kote.

### Jumanne 21

Umoja wa Kanisa siyo mwisho tu, bali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kama ishara, chombo na matunda ya kwanza ya lengo lake la kupatanisha vitu vyote mbinguni na duniani kupitia Kristo. Azimio la Swanwick 1987

### Jumatano 22

Bwana, tunaomba utusamehe kwa wakati sisi kama Ushirika wa Akina Mama na pia makanisa, tumenena maneno matupu kwa ajili ya umoja wa Kikristo bila nia yetu kuonekana katika mtazamo na utekelezaji. Badilisha miyo yetu ili tuweze kuwa na umoja wa kweli katika upendo wa Kikristo.

### Alhamisi 23

Baba wa daima, tunakusifu kwa kutuma Mwana wako kuwa mmoja wetu na kutuokoa sisi wote. Angalia juu ya watu wako kwa rehema, kwa maana sisi tumegawanyika kwa njia nyingi, na utupe Roho yake Yesu kutufanya kitu kimoja katika upendo.

### Ijumaa 24

Siku ya leo tunaombea umoja wa makanisa katika maeneo yetu ya ndani, na tunatoa shukrani kwa juhudii tunazoshirikia pamoja.

### Jumamosi 25

"Kwa sasa, ndugu, kwaherini! Muwe na ukamilifu, shikeni mashauri yangu, muwe na nia moja; kaeni kwa amani. Naye Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. 2 Wakorintho 13:11

#### Wimbi la Maombi

**Januari 19-21:** St Mark the Evangelist, Afrika Kusini; Butare, Rwanda; Okigwe-South, Nijeria; Gambia; British Columbia, Kanada na Rajasthan, India

**Januari 22-24:** Misri; Gasabo, Rwanda; Otukpo & On the Coast, Nijeria; Bathurst, Australia na Nasik, India

## Umaskini na ukosefu wa makazi Jan 26 - Feb 1 2020

### Jumapili 26

Tunawaombea wale ambao wanakabiliwa na uhaba wa umaskini, ukosefu wa makazi au kufukuzwa kwa makazi yao. Tunataka sisi kama wanachama wa Ushirika wa Akina Mama tutie changamoto dhidi ya udhalimu, tena tufanye kampeni ya kuleta mabadiliko ya kuboresha jamii zetu zote.

### Jumatatu 27

Shuka, Roho Mtakatifu, jaza miyo ya watu wako na uwashe moto wa upendo wako ndani yetu.

### Jumanne 28

Tuwe maskini au matajiri, tunaomba kwamba maneno yetu na matendo yetu yaweeze kuangaza kwa haki na kwa matumaini kwa njia ya kutimizwa kwa mchakato wetu wa MULOA. Bwana, tusaidie kuonyesha upendo wako kwa wote.

### Jumatano 29

Bwana tunawaombea wale ambao walilala mitaani jana usiku, wale ambao hawakuweza kulala kwa kuhofia kwamba hii itakuwa hatima yao hivi karibuni, wale ambao walilala katika baridi, kwa hali ya unyevunyevu bila joto, na wale ambao walikwenda bila chakula ili waweeze kuwalisha na kuwapamba nguo watoto wao.

### Alhamisi 30

Leo tunaombea kazi ya wanachama wetu ya kupunguza umaskini na kuwasaidia wenye shida ya makazi. Tunaomba kwamba wanapotoa kwa ajili ya wengine, waweze kupokea kiburudisho na upya katika nguvu za Roho Mtakatifu.

### Ijumaa 31

Naomba Mungu, ambaye aliacha makao yake ya utukufu, ahurumie wote wanaoishi duniani bila pahali wanapoweza kuita nyumbani. Mungu, ambaye hakuwa na mahali pa kupumzikia, awatetee na awape kimbilio. Amina

## FEBRUARI

### Jumamosi 1

Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo? Watoto wapendwa, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa vitendo naukweli. *Yohana 3:17-18*

### Wimbi la Maombi

**Januari 26-28:** False Bay, Afrika Kusini; Shinyanga, Tanzania; Umuahia & Ijebu South West, Nijeria; Bath & Wells, Uingereza na Vellore, India

**Januari 29-31:** Masvingo, Zimbabwe; Kilondo, Tanzania; Nebbi, Uganda; Bida, Nijeria; Llandaff, Wales na Kanyakumari, India

## Kuishi kwa Imani

## Februari 2-8 2020

### Jumapili 2

Baba wa mbinguni, najitolea mwenyewe katika huduma yako kama ishara ilio hai ya Utukufu wako maishani mwangu. Naomba ya kwamba vitendo vyangu vyote viwe vimejengwa juu ya upendo wako na vipate kibali mbele zako. Amina

### Jumatatu 3

Bwana wa imani, kama vile mfinyanzi na udongo, najtoa mwenyewe katika mikononi yako siku ya leo ili unifinyange na uninyooshe niwe mtu ambaye uliyounda.

### Jumanne 4

Katika imani, nathibitisha kwamba Mungu ameniumba kwa madhumuni ya kushiriki katika kuthibitisha upendo wake duniani. Ninaomba anibariki kwa kila jambo jema ninalohitaji ili nitimize kazi yangu kwa ajili yake leo.

### Jumatano 5

Bwana Mungu utupendaye, tupe nguvu na ujasiri ambazo tunahitaji ili tuishi kwa mujibu wa imani yetu. Na tuwe chanzo cha kuwatia moyo wengine na mifereji ya amani na maridhiano katika ulimwengu wetu ulio na mashaka.

### Alhamisi 6

Mungu baba tunakushukuru kwamba wewe uko pamoja nasi wakati tunakumbwa na shida na njia ilio mbele yetu ni ngumu. Tupe nguvu ya kukabili mambo yajayo, salama katika ujuzi ya kwamba upendo wako hushinda yote. Tunataka kusisitiza nia yetu ya kushiriki na wewe ili hiari yako iweze kufanyika, chochote kilicho mbele yetu.

### Ijumaa 7

Tunashukuru kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama duniani kote ambao wanashiriki imani yao kwa njia ya vitendo. Tunaomba ya kwamba msingi wa imani ambao maisha yao yamejengwa juu yake, uzidi kukua na kupata nguvu kwa kila msimu unaopita.

### Jumamosi 8

Abrahamu hakuionea mashaka ile ahadi ya Mungu; alipata nguvu kutokana na imani, akamtuza Mungu. Alijua kwamba Mungu anaweza kuyatekeleza yale aliyahidi. *Warumi 4:20-21*

### Wimbi la Maombi

**Februari 2-4:** Matlosane Afrika Kusini; Mumias, Kenya; Eha-Amufu, Nijeria; Ballarat, Australia; Niagara, Kanada na North Kerala, India

**Februari 5-7:** Botswana; Marsabit, Kenya; Idah & Jebba, Nijeria; Salisbury, Uingereza na Andaman & Car Nicobar Islands, India

# Ushirika wa Akina Mama – Wanachama Milioni 4 Duniani



## Jumapili 9

Bwana, ambaye uliishi maisha ya familia katika Nazareti, tunakushukuru kwa ajili ya familia zetu na tunaomba tuweze kuishi kwa namna inayotafakari upendo wako katika uhusiano wetu.

## Jumatatu 10

Bwana, tusaidie katika majukumu yetu muhimu ya kutunza familia zetu, hasa kama tuna watoto wa kulea. Tupe utambuzi siku baada ya siku hivyo kwamba, kwa nguvu zako, tutimize majukumu yetu yote vizuri.

## Jumanne 11

Tunawaombea akina mama na baba wanaolea katika familia zao wakiwa peke zao. Wawe na msaada wote wanaohitaji katika kuhudumia watoto wao, hasa wakati wanaokabiliwa na matatizo.

## Jumatano 12

Mungu wa huruma, tunaombea familia zinazokibiliwa na matatizo fulani kwa njia ya ukosefu wa ajira, umaskini au ugonjwa. Lete pamoja nao wale amba wana weza kuwasaidia, nasi tuweze kutambua na kutenda tunapopata nafasi za kupunguza mizigo yao.

## Alhamisi 13

Tunaombea mipango yote ya Ushirika wa Akina Mama ambayo inahamasisha kwa kikamilifu maisha ya jamii iliyo imara na kusaidia watu walio katika hali ya upweke na mazingira magumu. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya mabadiliko ambayo yanafanya kwa watu binafsi, familia na jamii katika nchi nydingi.

## Ijumaa 14

Asante, Bwana, kwa marafiki zetu. Tufanye tuwe msaada sisi kwa sisi, tushiriki katika furaha na huzuni yetu, tuhamasishane na tuwezavyo tuongozane kwa njia ya uzoefu wetu pamoja.

## Jumamosi 15

Marafiki wengi waweza kumwangusha mtu, lakini wapo marafiki waaminifu kuliko ndugu. *Methali 18:24*

### Wimbi la Maombi

**Februari 9-11:** Lainya, Sudan Kusini; **Ankole**, Uganda; **Abuja & Lagos-West**, Nijeria; **Lichfield**, Uingereza na **Karnataka North**, India

**Februari 12-14:** Matana, Burundi; **South Ankole**, Uganda; **Morogoro**, Tanzania; **Ohaji/Egbema**, Nijeria; **New Westminster**, Kanada na **Dornakal**, India

## Jumapili 16

Baba wa mbinguni, tunaomba kwamba utakuwa msingi wetu wa hakika leo na siku zote. Tupe nguvu ya kuwa imara katika imani yetu, licha ya vikwazo ambazo tunaweza kukutana nazo katika safari yetu.

## Jumatatu 17

Tunashukuru kwa uthabiti wa wanachama wetu wanaohusika katika hali ya vita na migogoro duniani kote. Tunamsifu Mungu kwamba hata wengine wakiondoka wao hubaki huku wakiwa kama ushahidi mkamilifu wa upendo wa Kristo.

## Jumanne 18

Basi Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, na kuhani mkuu wa milele mwenyewe, Mwana wa Mungu Yesu Kristo, awajenge kwa imani na ukweli na kwa unyenyekevu, na kwa uhuru wote dhidi ya hasira, na uvumilivu na subira na kustahimili na utakatifu. *Polycarp, 69-155 AD, Askofu wa Smirna*

## Jumatano 19

Bwana wa rehema tunatoa shukrani kwamba msingi wa muungano wetu ni imani, na kwa ajili ya uthabiti wa wanachama wetu amba hawageukii kando matatizo yanapotokea lakini huendelea kuwasaidia wenye shida katika dunia yako.

## Alhamisi 20

Baba tunawaombea Wakristo wanaoteseka kote duniani yako. Tunaomba kwamba wawe imara katika roho na kwamba wao watauhisi upendo wako huku ukiwainua na kuwashikilia.

## Ijumaa 21

Tunaomba leo kwa ajili ya wote amba wanajitahidi kusimamia imara hatua ya ukweli, lakini wanayumbayumba kwa sababu ya upinzani wa wengine. Tunaomba ili waimarishwe na upendo na faraja ya Kristo.

## Jumamosi 22

Basi, ndugu zangu wapenzi, simameni imara na thabiti. Endeleeni daima kuwa na bidii katika kazi ya Bwana, mkijua kwamba kazi mnayofanya katika utumishi wa Bwana haitapotea bure. *1 Wakorintho 15:58*

### Wimbi la Maombi

**Februari 16-18:** Bentiu, Sudan Kusini; **Bunyoro Kitara**, Uganda; **Okigwe-North & Omu- Aran**, Nijeria; **Kilmore, Elphin & Ardagh**, Ireland Yote na **Krishna-Godavari**, India

**Februari 19-21:** Free State, Afrika Kusini; **Bondo**, Kenya; **Ogbia & Offa**, Nijeria; **Swansea & Brecon**, Wales; **Argentina** na Uruguay

## Jumapili 23

Bwana, umetupa dunia ya ajabu. Tuongoze ili tutumie zawadi zako kwa busara, ili watu wote waweze kufurahia sehemu ya haki sawa ya yako.

## Jumatatu 24

Bwana, tunakushukuru kwa maono ya wale wote ambao mwaka 1992 walanzisha "Fair Trade Foundation" (Taasisi ya Biashara ya Haki) na kwa ushawishi wake wa kimataifa. Tunawaombea mafanikio duniani ili watu wote wapate haki kwa biashara hii.

## Jumanne 25

Tunaomba kwamba serikali zote zitambue ufahamu wa umuhimu wa biashara ya haki na kuendeleza utendaji bora na bei za haki katika jithada zao za kuinua uchumi kwa haki.

## Jumatano 26 Jumatano ya Majivu

Tunapoanza msimu wa maandalizi kwa ajili ya furaha ya Pasaka, hebu tutafakari juu yanjia zetu za dhambi na tuombe ili tupate msamaha. Bwana utupendaye, tunakuomba utufundishe kuishi maisha ya kawaida ili tuwape wengine nafasi ya kuishi.

## Alhamisi 27

Tunashukuru kwa kazi ya wanachama wetu ya kutekeleza maadili ya biashara ya haki huku wakisaidia watu binafsi, familia na jamii kufikia uwezo wao wote na kuchukua udhibiti wa maisha yao kwa heshima. Tunaomba kwa ajili ya kazi yao ya ulinzi wa mazingira, kwamba kilimo kiweze kushamiri licha ya changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

## Ijumaa 28

Bwana, tupe ujasiri wa kuijiliza kama chakula na mavazi tunayofikiri tunayahitaji katika maisha yetu inamaanisha kwamba wengine watakumbwa na njaa na unyonyaji, na uharibifu wa utamaduni wao na maisha yao. Tusaidie kuomba na kutumia maduka ambayo huuza bidhaa mbalimbali za biashara ya haki.

## Jumamosi 29

Mwadilifu anajua haki za maskini,lakini mtu mwovu hajui mambo hayo.

*Methali 29:7*

## Wimbi la Maombi

**Februari 23-25:** Wau, Sudan Kusini; **Kigeme**, Rwanda; **Bauchi**, Nijeria; **St David's**, Wales na **Mandalay**, Myanmar

**Februari 26-28:** Mundri, Sudan Kusini; **Madi & West Nile**, Uganda; **Isikwuatu**, Nijeria; **Chichester**, Uingereza na **Seoul**, Korea Kusini

## MACHI

### Jumapili 1

Ee Mungu, wewe u Mungu wangu, nami nakutafuta kwa moyo; roho yangu inakutamani kama mtu mwenye kiu; nina kiu kama nchi kavu isiyo na maji.

*Zaburi 63: 1*

### Jumatatu 2

Bwana, tunatambua msimu huu kama wakati wa ibada, lakini hakuna haja uwe wakati wa huzuni. Tusaidie kuutumia katika njia halisi, huku tukikuza ufahamu wetu kukuhusu wewe kupitia sala na kujifunza, kuwa tayari kusherehekea kwa furaha Pasaka tukufu.

### Jumanne 3

Bwana, uliamua kutumia uwezo wako kwa ajili ya kutenda mema kwa wengine tu bali sio kwa manufaa yako mwenyewe. Tusaidie, pia, kutumia kwa kuwajibika ushawishi wowote tulio nao juu ya watu wengine.

### Jumatano 4

Tunawaombea wale wanaopitia majoribu, wanaohisi wametengwa walio na udhaifu. Bwana, uwaonyeshe kwa uhakika uwepo wako, upendo wako na nguvu zipate kuwajia kwa wakati huu, waingie katika nafasi bora zaidi.

### Alhamisi 5

Tunawaombea wanachama wetu duniani kote kwamba wakiwa katika kazi zao, pia wawe na muda wa kusitisha, kumkaribia Mungu na kutafakari wakati wa msimu huu wenye thamani.

### Ijumaa 6 Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Wanawake

Mwenyezi Mungu, Mungu wa matumaini, tunawaombea wanawake na wasichana leo ili wawe yote wanayoweza kuwa. Tupe ujasiri wa kusema na kutafuta usawa na haki, mpaka dunia ijae uadilifu na upendo. Amen © Church of England

### Jumamosi 7

Bwana, wewe ulipata ushindi juu ya majoribu huko jangwani; tusaidie kipingana na majoribu ya kutenda maovu. Tupe neema ya kujuua matakwa yako kwa ajili yetu utupe nguvu ya kuishi kwa mujibu wa mapenzi hayo.

## Wimbi la Maombi

**Machi 2-4:** Yei, Sudan Kusini; **Luweero**, Uganda; **On the Lake**, Nijeria; **Grafton**, Australia; **Armagh**, Ireland-Yote na **South Kerala**, India

**Machi 5-7:** Bujumbura, Burundi; **Maseno South**, Kenya; **Ihiala**, Nijeria; **Kameruni**; **Calgary**, Kanada, na **Ysabel**, Visiwa vya Solomon

## Jumapili 8

Madaha huhadaa na uzuri haufai,bali mwanamke amchaye Mwenyezi-Mungu atasifiwa. *Methali 31:30 (Ujumbe)*

## Jumatatu 9

Bwana utupendaye, Mwana wa Maria, tunatoa shukrani leo kwa ajili ya wanawake katika familia zetu na mionganini mwa marafiki zetu ambao wametutunza na kutuongoza. Tunaomba leo kwamba kila mmoja wao ajue kwamba yeye anapendwa na anathaminiwa.

## Jumanne 10

Bwana utupendaye, tunatoa shukrani leo kwa ajili ya wanawake ambao kazi yao inagusa na kuimarisha maisha yetu. Kila mwanamke ambaye maisha yake yametuletea baraka ajue leo kwamba yeye anapendwa na anathaminiwa.

## Jumatano 11

Bwana utupendaye, tunaomba leo kwa ajili ya wanawake ambao juhudhi yao haionekani na kazi yao haitambuliwi. Tunaombea leo kila mwanamke ambaye amekaa kimya, yule asiyeonekana, ili ajue ya kwamba yeye anapendwa na anathaminiwa.

## Alhamisi 12

Bwana utupendaye, leo tunaombea wanawake ambao hukutana na vipingamizi na ubaguzi na kunyimwa kwa sababu ya jinsia yao. Mipaka yote ivunjwe ambayo inawazuia kustawi na kila mmoja wao ajue kwamba yeye ni mtu wa thamani

## Ijumaa 13

Bwana utupendaye, tunajiombea sisi wenyewe, utufunue macho na masikio wazi ili tugundue mahali ambapo mwanamke tunayemjua anahitaji faraja leo, tuweze kumletea faraja hio. Tupe ujasiri kila siku ili tuthibitishe thamani ya wanawake wote tunaowajua, kwa njia ya maneno na matendo yetu.

## Jumamosi 14

Chukua muda leo kutafakari kwa shukrani juu ya wanawake ambao wamesaidia kubadilisha maisha yako, wale ambao unwajua binafsi na wale ambao wamekuwa vielelezo wakiwa mbali.

### Wimbi la Maombi

**Machi 9-11:** Awerial, Sudan Kusini; **Mityana**, Uganda; **Uyo & Ajayi Crowther**, Nijeria; **Rupert's Land** Kanada na **Patna**, India

**Machi 12-14:** Port Elizabeth Africa Kusini; **West Ankole**, Uganda; **Nomadic Mission & Ekiti-Kwara**, Nijeria; **Worcester**, Uingereza na **Kanisa la Kianglikana la Ufilipino**

## Jumapili 15

Mungu atasuluhisha mizozo ya mataifa, atakata mashauri ya watu wengi. Watu watafua panga za vita kuwa majembe na mikuki yao kuwa miundu ya kupogolea. Taifa halitapigana na taifa lingine wala hayatafanya tena mazoezi ya vita.

*Isaya 2: 4*

## Jumatatu 16

Tupe yote, Baba, maono ya amani na maridhiano na kutusaidia kufuata njia yako ya upendo kwa kila mmoja kama ulivyo amuru tufanye. Wale walio madarakani watambue kwamba ukarimu kati ya maataifa utaleta heshima zaidi na pia maelewano katika dunia.

## Jumanne 17

Tunawaombea UNCSW mwaka huu wanapofikisha miaka mitano hatuani katika kufikia Malengo ya Maendeleo endelevu. Kila mahali, watu watambue upesi, usawa wa kijinsia na uvezeshaji wa wanawake na wasichana kila mahali.

## Jumatano 18

Bwana, tusaidie kumaliza uroho, hofu na chuki. Kila taifa lioneshe heshima kwa utofauti wa watu katika ulimwengu na tuwe tayari kujifunza kutoka kwa kila mmoja.

## Alhamisi 19

Baba, ongoza wale wanaohusika na Umoja wa Mataifa. Wape hekima wanapotafuta njia za kuleta amani na haki duniani kote.

## Ijumaa 20

Tunamshukuru Mungu kwa uwakilishi wa Ushirika wa Akina Mama katika UNCSW na kuomba kwamba sauti yetu tofauti isikike wazi wakati wa majadiliano na maamuzi yatakayofanyika mwaka huu.

## Jumamosi 21

Twaomba kwamba mataifa yote yaonyeshe heshima kwa manufaa yale dunia yetu inatutolea. Utusaidie kutumia rasilimali kwa faida ya wote; na kuondoa migogoro huku tukiziunga mkono nchi ambazo hazina mali nyingi ya kugawana kati ya raiya wao.

### Wimbi la Maombi

**Machi 16-18:** Kajo-Keji, Sudan Kusini; **Tarime**, Tanzania; **Dutse & Akoko-Edo**, Nijeria na **Canterbury**, Uingereza

**Machi 19-21 :** Antisiranana, Madagaska; **Busoga**, Uganda; **Yola & Oke-Ogun**, Nijeria; **Algoma**, Kanada na, **Jabalpur**, India

### Jumapili 22 Jumapili ya Uzazi

Atalilisha kundi lake kama mchungaji, atawakusanya wanakondoo mikononi mwake, atawabeba kifuan i pake, na kondoo wanyonyeshao atawaongoza polepole. *Isaya 40:11*

### Jumatatu 23

Baba wa Mbinguni, tunatoa shukrani kwa wale amba wametulea katika imani, walioituwezesha kukua katika upendo na uelewaji. Tunaomba nasi pia tuweze kuwalea wengine katika imani yao na kuwa chanzo cha Baraka kwa wale walio katika safari yao ya Kikristo.

### Jumanne 24

Tunashukuru leo kwa ulezi wa vipawa na vipaji ndani ya Ushirika wa Akina Mama. Tena Tunaomba kwamba fursa ifunguliwe kwa ajili ya wanachama ili wastawi na kukua katika yote ambayo Mungu anawaita wafanye.

### Jumatano 25 Siku ya Maria

Ee Bwana Yesu Kristo tunaomba utupe, neema za Maria; imani, uvumilivu, utii, shukrani na ujasiri.

### Alhamisi 26

Kazi ya meneja inahusu kupanga na kuarifu. Ya kiongozi inahusu kulea na kuimarisha. Tom Peters, Mtendaji Mmarekani. Bwana, kwa njia yoyote tunayoweza, tupate kulea na kuimarisha wale amba tunawaongoza..

### Ijumaa 27

Bwana wa Rehema tunatoa shukrani kwa ajili ya mafanikio ya Uzazi wa Mpango kote duniani, na kwa ajili ya wale wamejifunza kulea familia zao kwa kupanda mbegu za upendo na huduma ambazo zinaweza kukua na kufikishwa kwa vizazi vivitakavyofuata.

### Jumamosi 28

Tunawaombea watoto wote wanaishi katika sekta ya huduma. Tunashukuru kwa walezi amba hulea watoto wa watu wengine katika huduma yao, na kuwapa makazi ambapo wanaweza kupata usalama, upendo na kujisikia sehemu ya familia.

### Wimbi la Maombi

**Machi 23-25:** Rokon, Sudan Kusini; **Kampala**, Uganda; **Kaduna**, Nijeria; **Koforidua**, Ghana; **Brisbane**, Australia na **Peru**

**Machi 26-28:** Central Zambia, Zambia; Southern Highlands, Tanzania; Ogburu & Badagry, Nijeria; **Bermuda** na **Chandigarh**, India

### Jumapili 29

Hata hivyo, Mwenyezi-Mungu anangoja awafadhili, atainuka na kuwaonea huruma. Maana, Mwenyezi-Mungu ni Mungu atendaye haki. Heri wote wale wanaomtumainia. *Isaya 30:18*

### Jumatatu 30

Mwenyezi Mungu, maana wewe ni Mungu wa haki, tusaidie tuweze kuwa watu wako kwa haki. Utujaze huruma kwa watu masikini. Kwa kila sisi tunachofanya kiwe na mizizi ya uaminifu na uadilifu.

### Jumanne 31

Tunaombea leo, wale wote amba huendeleza haki katika serikali, katika kanisa na kwa jamii zao. Sauti zao zisikike wazi na kubainishwa kupita kelele za ajenda nyingine.

### APRILI

#### Jumatano 1

Baba wa mbinguni, tunakushukuru kwamba rehema zako ni mpya kila asubuhi. Tunataka kuthamini uhuru tunaoujua kwa neema yako, na kuwa watu amba huonyesha haki na huruma kwa wengine.

#### Alhamisi 2

Mungu atubariki tupate hasira tunapoona udhalimu, uonevu, na matumizi mabaya ya watu, ili tuweze kufanya kazi kwa uadilifu, uhuru na amani. *Barikisho la Kifrancisco*

#### Ijumaa 3

Bwana Mungu, tupatia maono ya dunia yako kama vile upendo wako ungetaka iwe: ambapo wadhaifu wanalinwa, na hakuna hata njaa wala umaskini; ambapo jamii za tamaduni mbalimbali zinaishi kwa amani na kuheshimiana; ambapo amani imejengwa kwa haki, na haki inaongozwa na upendo.

#### Jumamosi 4

Ee Bwana, fungua macho yangu nipate kuona mahitaji ya wengine; masikio yangu nipate kusikia kilio chao; moyo wangu ili wasije wakawa bila msaada. Nionyeshe pale ambapo upendo, matumaini, na imani zinahitajika, ili mimi niwe na uwezo wa kufanya baadhi ya kazi ya amani na haki kwa ajili yako.

### Wimbi la Maombi

**Machi 30-Aprili 1:** Toamasina, Madagaska; **Mukono**, Uganda; **Ikwerre & Ife East** Nijeria; **Down & Dromore**, Ireland Yote, na **Delhi**, India

**April 2-4:** Umzimvubu, Afrika Kusini; **Lweru**, Tanzania; **On the Niger**, Nijeria; **Cape Coast**, Ghana; **Ontario**, Kanada na **Limerick & Killaloe**, Ireland Yote

## Juma Takatifu

5-11 Aprili 2020

### Jumapili 5 Jumapili ya matawi

Shangilieni sana enyi watu wa Sayuni! Paazeni sauti, enyi watu wa Yerusalem! Tazama, mfalme wenu anawajieni, anakuja kwa shangwe na ushindi! Ni mpole, amepanda punda, mwanapunda, mtoto wa punda. Zekaria 9: 9

### Jumatatu 6

Tunapotafakari juu ya matukio makubwa ya Juma takatifu hebu tutamani kuwa mashahidi wa Yesu kwa wale walio karibu nasi, iwe Wakristo wenzetu ama wale wasio na imani, ili watu zaidi wapate kujua upendo wake Kristo kwao wenyewe.

### Jumanne 7

Vile Maria alimpaka Yesu mafuta kama kitendo cha upendo na huduma, na sisi tuwe tayari kusikiliza ushawishi wa miyo yetu na kutafuta njia mpya za kumpenda na kumtumikia Bwana wetu.

### Jumatano 8

Mungu Baba yetu wa Mbinguni, tunakuabudu kwa upendo wako wa kafara; kwa vile ulitoa Mwana wako mpendwa katika tendo la thamani la kutukomboa, ambalo lilituletea maisha kwa miyo yetu na matumaini milele kwa ulimwengu.

### Alhamisi 9 Alhamisi Kuu

Usiku huu, Yesu aliosha miguu ya wanafunzi wake, kama mfano wa utumishi wenye upendo. Tusaidie kutendea wengine kama aliviyotutendea sisi. Uimarishie mikono yetu na roho zetu ili tufuate mapenzi yake kwa upendo.

### Ijumaa 10

Jemadari mmoja aliyejewa amesimama mbele yake alipoona jinsi Yesu alkata roho, akasema, "Kweli mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu!" Marko 15:39  
Mwana wa Mungu, tunasimama mbele ya msalaba tukikuabudu. Amina

### Jumamosi 11

Bwana tunatua kwa muda na kutafakari katika utulivu huku ulimwengu unaposubiri mwanzo wa kufufuka kwake. Uchungu wa msalaba umepita; furaha ya maisha mapya imekaribia; miyo yetu imejaa ajabu na shukrani kwa Mungu.

### Wimbi la Maombi

**April 6-8:** Cueibet, Sudan Kusini; Gahini, Rwanda; Wusasa & Ibadan, Nijeria na Christchurch, Nyuzilandi

**April 9-11:** Nord Kivu, Kongo; Kigali, Rwanda; Kiteto & Kubwa, Nijeria; Perth, Australia na Kuranagala, Sri Lanka

## Kristo Amefufuka!

12-18 Aprili 2020

### Jumapili 12 Jumapili ya Pasaka

Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Kwa rehema yake kuu yeye ametupa kuzaliwa upya ili tupate tumaini hai kuitia ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu. 1 Petro 1: 3

### Jumatatu 13

Huku tukifurahia ufufuo wa Kristo, tunatoa shukrani kwa ajili ya wanawake wajasiri ambaao walikimbia hadi kaburini na kisha wakarudisha habari za ajabu. Tunaombea wanawake walio na ujasiri wa kuongoza katika jamii zao wenyewe ili kuleta maisha mapya.

### Jumanne 14

Msalaba ndio ushindi, ufufuo ndio shangwe . ufufuo ni kuonyesha ushindi hadharani, ushindi wa yeye aliyesulubiwa. *Eric Sauer, Mwana-theologia, 1898-1959*  
Tunamsifu Mungu kwa ushindi wa milele wa ufufuo.

### Jumatano 15

Katika mshangilio na furaha ya Pasaka tunakumbuka wale ambaao huu ni wakati mgumu kwao, kwa sababu yoyote ile. Tunaomba kwamba wale ambaao bado wanaishi katika giza wapate mwanga na maisha mapya hivi karibuni.

### Alhamisi 16

Tunashukuru kwa wakati wale katika maisha yetu tumekuwa na uzoefu wa ufufuo. Hebu tutafakari juu ya umuhimu wa wakati huo na tusaidie wengine kupata uzoefu wao wenyewe wa kufufuka kwake.

### Ijumaa 17

Bwana yuko hai; Tumepata matumaini mapya. Hofu imeshindwa; mustakabali wetu ni wa milele. Halleluya. Kristo amefufuka nasi tutafufuka pamoja naye. Mungu asifiwe kwa ishara ya ufufuo.

### Ijumaa 17

Tunaomba kwa ajili ya wale wote waliobatizwa au waliothibitisha imani yao katika wakati wa Pasaka, kwamba wakiwa katika mwanzo wa maisha mapya na kuendelea na safari yao ya Kikristo, wazidi kumkaribia Mungu, siku baada ya siku. Wasaidie kupata marafiki ambaao watashiriki nao katika maisha yao ya kiroho.

### Wimbi la Maombi

**April 13-15:** Yirol, Sudan Kusini; Ruvuma, Tanzania; Nike & Benin, Nijeria; Canberra & Goulburn, Australia na Dogura, Papua New Guinea

**April 16-18:** Kindu, Kongo; Mount Kenya West, Kenya; Egbu, Nijeria; Te Pihopatanga O Aotearo, Nyuzilandi; Cork, Cloyne & Ross, Ireland Yote na Eastern Himalayas, India

## Jumapili 19

Kumbuka kuwa mimi nimekuamuru uwe imara na hodari. Usiogope wala usifadhaike kwa kuwa mimi Mwenyezi-Mungu, Mungu wako, niko pamoja nawe popote uendapo *Yoshua 1: 9*

## Jumatatu 20

Tunashukuru leo kwa ujasiri na ushahidi wa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama wanaofanya kazi katika hali ya hatari na tunawaombea ulinzi wa Mungu dhidi ya madhara na upinzani kwa kazi yao.

## Jumanne 21

Tunapokutana na mashaka, tunamsifu Mungu kwamba yeye hutupa nguvu na amani ya akili ili tusonge mbele kwa ujasiri. Tunamshukuru kwamba hakuna hali ambayo ni ngumu sana kwake, ambayo asiyoweza kutupitisha.

## Jumatano 22

Baba wa Mbinguni tunawaombea watoto kila mahali, kwamba utawawezesha kuendelea maishani yalio mbele yao kwa ujasiri, uamuzi na uvumilivu.  
(*1 Wakorintho 9: 24-27*)

## Alhamisi 23

Imani inaweza kutupatia ujasiri wa kuwa na uhakika katika maisha ya baadaye. *Martin Luther King Jr.* Bwana tunaomba kwamba imani yetu izidi hofu na iwe imejengwa juu yake Kristo, ili tuweze kukabili kishujaa jambo lolote lililo mbele yetu.

## Ijumaa 24

Wanachama wetu wengi wanaishi maisha magumu. Neema ya Mungu ifunike miyo yao kwa amani na kuwajaza ujasiri kwa kila siku wanaposhiriki upendo wa Kristo katika maisha yao ya matendo maaminifu.

## Jumamosi 25

Bwana Yesu katika nyakati za maisha yetu ambazo sisi hasa tunahitaji ujasiri wako, tunakushukuru kwa miujiza unayotenda ili tuweze kufanya matendo ya ajabu katika imani, siku kwa siku.

## Wimbi la Maombi

**April 20-22:** Kinshasa, Kongo; Victoria Nyanza, Tanzania; Ahoada & Warri, Nigeria; Oxford, Uingereza na Port Moresby, Papua New Guinea

**April 23-25:** Kisangani, Kongo; Kager, Tanzania; Awkain, Nigeria; Sunyani, Ghana; Manchester, Uingereza na Popondot, Papua New Guinea

## Jumapili 26

Bali mnnapaswa kuwa watakatifu katika mwenendo wenu wote, kama vile yule aliyewaiteni ni mtakatifu. Maandiko yasema: "Muwe watakatifu, kwa kuwa mimi mtakatifu." *1 Petro 1: 15-16*

## Jumatatu 27

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, wewe ni Bwana Mungu Mwenyezi. Bwana tusaidie kufuata mfano wako maishani mwetu, tuweze daima kufikiria wengine na mahitaji yao.

## Jumanne 28

Baba Mtakatifu, utupe hekima ya kutambua uwepo wako katika maisha yetu, na kuelewa kile unachotaka tufanye. Tuma Roho wako Mtakatifu kwetu na ututenge sisi mbali na dunia, ili tuishi maisha matakatifu kama Yesu anavyotaka.

## Jumatano 29

Mwenyezi Mungu, Kanisa lako katika ulimwengu mzima litafakari utakatifu wako na liangaze kama vile mwangaza katika ulimwengu wa giza. Kila moja ya makanisa lirudishe nuru ya utakatifu wako na lijulikane kwa kumeremeta upendo wa Kristo.

## Alhamisi 30

Bwana, tuonyeshe leo furaha ya utakatifu; faida kubwa ya kuishi kama watu wako, waliotengwa kutoka dunia, tukitamani nguvu za Roho Mtakatifu zifanye kazi ndani yetu kwa kuzalisha maadili na tabia yenyе kumcha mungu.

## MEI

## Ijumaa 1

Kama unafikiri unaweza kutembea katika utakatifu bila kutunza ushirika wa daima pamoja na Kristo, umefanya makosa makubwa. Ukitaka kuwa mtakatifu, lazima uishi karibu na Yesu. *Charles Spurgeon, 1834-1892, Mhubiri wa Kibaptisti.* Bwana utupendaye, tuvute na utuweke karibu na Kristo. Amina

## Jumamosi 2

Bwana, wakati unatuita kwa utumishi wako, tafadhalii tusaidie kudumu katika kazi uliyotutuma, ili tuweze kufikia mwisho wa safari yetu kwa amani na utakatifu wako.

## Wimbi la Maombi

**April 27-29:** Port Sudan, Sudan Kusini; Muhabura, Uganda; Niger Delta West & Yewa, Nigeria; The Northern Territory, Australia na Chennai, India

**April 30-Mei 2:** Aru, Kongo; Kigezi, Uganda; Ikeduru, Nigeria; Ho, Ghana; York Uingereza na Guyana & Suriname, Guyana

### Jumapili 3

Kama mkitii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, mtapewa baraka zifuatazo; Miji yenu itabarikiwa na mashamba yenu. *Kumbukumbu 28: 2-3 (NIRV)*

### Jumatatu 4

Tusaidie, Bwana, kutambua baina ya utegemezi kati ya uzalishaji katika maeneo ya vijiji, na masoko na biashara katika maeneo ya mijini, tusababishe viunganisho vyenye maendeleo yatakayojenga uchumi wa ndani na ukuaji katika majimbo.

### Jumanne 5

Watu wote popote wanapoishi duniani, Mwimbieni Bwana kwa sauti ya furaha [A & M 166] Baba utupendaye, sisi ni watu wako wote popote tunapoishi, kwa hivyo tufuate mfano wako wa upendo na Amani, kisha tuishi pamoja kwa upatanifu.

### Jumatano 6

Asante Bwana kwa teknolojia ya kisasa; tunaomba kwamba matumizi yake yatuletee mawasiliano bora zaidi, na ufahamu mkubwa zaidi wa shida zinazokibili jamii mbali mbali. Tena teknolojia hii isaidie makampuni kukuwa katika maeneo yote.

### Alhamisi 7

Leo tunawaombea wote wanaofanya kazi na jamii maskini katika maeneo ya mijini na vijiji. Tunaomba wapate mawazo mazuri, na serikali ziwe na msimamo wa kisasa katika kukabiliana na mizizi ya umaskini uliopo mijini na mashambani.

### Ijumaa 8

Bwana, tunaihi katika jamii, tamaduni na familia tofauti, lakini tunaunganishwa katika imani na maombi. Tunaomba tufahamu zaidi mahitaji ya kila mmoja, huku tukiendelea kuonyesha imani yetu kwa vitendo ili tulete mabadiliko katika dunia yako.

### Jumamosi 9

Fikiria leo eneo la kijijini au mjini ambalo ni maalum kwako. Omba kwa ajili ya wale wanaoishi katika eneo hilo, ya kwamba watafurahia uzuri wa maisha katika eneo hilo na watazikibili changamoto zilizopo.

### Wimbi la Maombi

**Mei 4-6:** Uppershire, Malawi; Maralal Missionary Area, Kenya; Makurdi & Ifo, Nijeria; Tuam, Killala & Achonry, Ireland Yote na Mumbai, India

**Mei 7-9:** Torit, Sudan Kusini; Meru, Kenya; Ikwuano, Nijeria; Sekondi, Ghana na The Arctic, Kanada

### Jumapili 10

Furahini daima, salini kila wakati na kuwa na shukrani katika kila hali. Hayo ndiyo anayotaka Mungu kwenu katika kuungana kwenu na Kristo Yesu.

*1 Wathesalonike 5: 16-18*

### Jumatatu 11

Mshangilieni, mwimbieni Mungu sifa; simulieni matendo yake ya ajabu! *1 Nyakati 16: 9* Bwana, tusaidie kujtiolea kwako kila siku kwa furaha, tukiju ya kwamba sisi ni wako na wewe ndiye mwenye nguvu juu ya mambo yote.

### Jumanne 12

Kila kiumbe hai kimsifu Mwenyezi Mungu! *Zaburi 150: 6* Mungu wa upendo, tunaomba tuwe na moyo wa shukrani unaoweka maisha yetu juu yako na kutusaidia kusimama imara kwa kila aina ya mazingira.

### Jumatano 13

Basi, Mungu wetu ni wa ajabu! Yeye ni yule yule leo kama vile mwanzo wa nyakati na ataishi milele! Hakuna tatizo kubwa mno au gumu mno ambalo hawezি kulishinda. Kwa hivyo tunaleta maombi yetu kwake leo tukimsifu na kumuabudu.

### Alhamisi 14

Bwana, tunakusifu, na kukushukuru kwa miujiza ambayo umefanya katika maisha yetu - ushahidi wetu na furaha yetu iwaongoze wengine kushereheke na kufurahia ufalme wako.

### Ijumaa 15

Bwana, huku tukileta shukrani na sifa zetu, tunawaombea wote walio na wasiwasi, katika hatari au mateso kutokana na ugonjwa au ulemavu. Tupe neema ya kuwasaidia wale tunakutana nao, walio katika aina yoyote ya mahitaji.

### Jumamosi 16

Bwana, tupe hekima na mtizamo ili tuweke maombi na sifa kama lengo kwa maisha yetu ili kwa furaha yetu sauti yako iweze kusikika mbali.

### Wimbi la Maombi

**Mei 11-13:** Twic East, Sudan Kusini; Rarya, Tanzania; Owerri & Ughelli, Nijeria; Gippsland, Australia na Cashel & Ossory, Ireland Yote

**Mei 14-16:** Maridi, Sudan Kusini; Kirinyaga, Kenya; Zaki-Biam & Ijesa North-East, Nijeria na Waikato & Taranaki, Nyuzilandi

## Jumapili 17

Namtumainia Mwenyezi Mungu kwa moyo wangu wote ; nina imani sana kwa neno lake. Ninamtumainia Mwenyezi Mungu kuliko walini wanavyongojea pambazuko; *Zaburi 130: 5-6*

## Jumatatu 18

Bwana tunawaombea kina mama waja wazito wanaosubiri kwa furaha na matumaini kuzaliwa kwa mtoto wao. Wape uvumilivu wakati wa kuzaa na ujasiri wanapoijitarisha kuchukua majukumu ya kuongoza mwanadamu mpya katika sura mpya ya maisha ya familia zao.

## Jumanne 19

Bwana wa huruma, kuwa na wote ambao wanaosubiri pembeni mwa kitanda cha wagonjwa. Wape uvumilivu na uhakika wa faraja inayoletwa kwa uwepo wao.

## Jumatano 20

Tusamehe Bwana, wakati tunakuwa na shaka tunaposubiri, na kutoamini mipango na madhumuni yako. Bwana wa utukufu, tukaribie na utesubiri kwa ustahamilivu mpaka tuje kwako. Unashiriki kusubiri kwetu katika upendo wako na kupafanya paiali pa neema.

## Alhamisi 21 Sikukuu ya kupaa Yesu Kristo mbinguni

Yesu huyu ambaye amechukuliwa kutoka kwenu kwenda mbinguni atakuja tena namna hiyo hiyo mlivyomwona akienda mbinguni. *Matendo 7:17* Tufurahi leo tuna-pomwona Yesu akirudi kwa Baba akiwa na ahadi ya kwamba atakuwa nasi siku zote. Asante Bwana kwa vile hakuna wakati kamwe tulio peke yetu tukikutegemea wewe.

## Ijumaa 22

Tunaomba leo kwa ajili ya wale wote wanaosubiri matokeo ya vipimo vyta matibabu, ili wajue amani ya Kristo ipitayo ufahamu wote, watibiwe kwa wema na huruma, matokeo yakiwa mema au mabaya.

## Jumamosi 23

Tunapongojea kuja kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste tunaomba tupate kuwa tayari kutangaza Kristo kama Bwana na Mfalme katika yote tunayofanya na kusema kila siku ya maisha yetu katika dunia hii.

### Wimbi la Maombi

**Mei 18-20:** Grahamstown, Africa Kusini; Masasi, Tanzania; Afikpo, Nijeria; Wiawso, Ghana; Chester, Uingereza na Argentina Kaskazini, Argentina

**Mei 21-23:** Christ the King, Africa Kusini; East Rwenzori, Uganda; Gombe & New Busa, Nijeria na Bunbury, Australia

## Jumapili 24

Wala hakuna atakayeweza kusema, 'Uko hapa', au 'Uko pale'. Kwa kweli ufalme wa Mungu uko kati yenu. *Luka 17:21*

## Jumatatu 25

Bwana Mungu, wewe daima uko nasi. Unajalia kila mmoja wetu katika ufalme wako hapa duniani. Tunakusifu kwa majibu yako mengi ya maombi ambayo yanakufikia kwa njia zisizotarajiwa. Amina

## Jumanne 26

Baba wa Mbinguni, hebu tuonyeshe watu kwamba ufalme wako u pamoja nasi wakati huu kwa kuonyesha maadili ya ufalme wako kuititia jinsi sisi tunavyosikiliza matatizo ya wengine, jinsi tunavyosikiliza mahitaji yao, na sio kuhukumu wengine bila huruma.

## Jumatano 27

Ufalme wa Mungu utaweza kuwa wazi katika ulimwengu huu kabla ya Kristo kurudi kwa njia moja tu, nayo ni kuititia jinsi sisi tunaishi kama raia wa mbinguni na watawaliwa wa Mfalme. *RC Sproul, 1939-2017, Mwana-Theologia wa kimarekani*

## Alhamisi 28

Baba wa mbinguni, Kanisa lako litangaze ufalme wako kwa maombi, huduma na Vitendov vyake kwa wale walio na njaa, wasiokuwa na makazi na wale walio katika mateso.

## Ijumaa 29

Bwana, tunakushukuru kwa kazi wanachama wetu wanayofanya ili kujenga ufalme wa Mungu katika sehemu yao iliyopo katika dunia yako. Tunaomba kuangaza kwao kuonyeshe maadili ya ufalme ili maisha imara ya familia yahamasishwe na jamii zibadilishwe.

## Jumamosi 30

Kristo Mfalme na Mwokozi wetu, tunakushukuru kwa kuangaza mwanga wa ufalme wako katika maisha yetu. Mwanga huo utuhamasishé ili tufanye kazi kwa shauku ya kuona ufalme wako hapa duniani.

### Wimbi la Maombi

**Mei 25-27:** Bor, Sudan Kusini; Mount Kilimanjaro, Tanzania; Oru & Oleh, Nijeria; Rockhampton, Australia na Agra, India

**Mei 28-30:** Angola; North Ankole, Uganda; Okene & Ibadan-South, Nijeria; Aberdeen & Orkney, Scotland na Karnataka South, India

## Jumapili 31 Pentekoste

Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapowashukieni nyinyi, mtapokea nguvu na mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, katika nchi yote ya Yudea na Samaria, na hata miisho ya dunia. *Matendo 1:8*

## JUNI

### Jumatatu 1

Shuka, Roho Mtakatifu, tulete kwenye njia ya ukweli. Maisha yetu yawe huru kutoka katika mambo yanayouzia imani katika maisha yetu ili tukupende na tukutumikie wewe katika utii wa kweli.

### Jumanne 2

Shuka Roho Mtakatifu. Jaza maisha yetu dhaifu yasiyo na maana, kwa nguvu na uwezo wako. Furisha maisha yetu yalio kame kwa mito ya maji ya uzima. Washa maisha yetu baridi kwa joto kubwa la moto mtakatifu.

### Jumatano 3

Kujaribu kufanya kazi ya Bwana kwa nguvu yako mwenyewe ni jambo la kutatanisha, kuchosha, na kutaabisha zaidi kuliko kazi zote. Lakini ukiwa umejazwa na Roho Mtakatifu, basi huduma ya Yesu inatiririka tu kutoka kwako. *Corrie Ten Boom, 1892-1983*

### Alhamisi 4

Shuka, Roho Mtakatifu, njoo kama upopo wa mawimbi na kujaza kila kipembe ya maisha yetu; tujaze uwepo wako wenye nguvu ili tujazwe na Roho na tuongozwe na Roho tunapotembea kila siku na wewe.

### Ijumaa 5

Shuka, Roho Mtakatifu, ujaze maisha yetu kwa nguvu ya uwepo wako. Tupe uwezo wa kufanya kazi yoyote, kubwa au ndogo, ambayo ni hiari yako kwetu.

### Jumamosi 6

Ingawa Roho kamwe haibadiliki, matokeo ya hatua ya Roho, kwa mapenzi ya Mungu na kwa jina la Kristo, ni mengi na ya ajabu. *Cyril wa Yerusalem*. Moto wa Mungu waka ndani yetu. Upopo wa Mungu tutie nguvu. Neno la Mungu tutie moyo. Mungu wa Pentekoste kuwa baraka kwetu leo na siku zote. Amina

### Wimbi la Maombi

**Juni 1-3:** **Johannesburg**, Afrika Kusini; **Kumi**, Uganda; **Nsukka & Idoani**, Nijeria; **Derby**, Uingereza na **Madhya Kerala**, India

**Juni 4-6:** **Ibba**, Sudan Kusini; **Maseno North**, Kenya; **Isiala-Ngwa & Ondo**, Nijeria; **Fredericton**, Kanada na **Amritsar**, India

## Jumapili 7

Mtu mkarimu atafanikishwa, amnyweshaye mwingine maji naye atanyweshwa. *Methali 11:25*

### Jumatatu 8

Mwito sio tu suala la kuwa na kufanya kile sisi tulicho, lakini pia ni jambo la kuwa kile bado hatujakuwa, ila tumeitwa na Mungu kuwa. *Os Guinness, Mwandishi*. Huku tukitokuza wafanya kazi wa kujitolea, ambao ni vyanzo vya matumaini na zawadi kwa watu wengi, tunaomba kwamba Kristo awe tegemeo ambalo daima linabadilisha na kuleta nguvu mpya kwa roho zao.

### Jumanne 9

Tunakushukuru sana kwa furaha na utulivu ambazo zinaletwa na wafanya kazi wa kujitolea. Wapate tegemeo na nguvu za kukabiliana na hali zote na wajue uwepo wako katika kila pambano.

### Jumatano 10

Leo tunatukuza miyo ya kujitolea ya wanachama wetu duniani kote, wanachama ambao kwa uaminifu wanakutumikia wewe kwa njia zisizoonekana kwa wengi, wale wanaotoa bila ubin afsi muda wao na zawadi zao ili wafuate amri yako ya kumpenda jirani yetu tunavyo jipenda wenyewe.

### Alhamisi 11

Mungu wetu, tunashukuru kwamba wakati tunapofanya kila kazi ikiwa kazi ya upendo, sisi huleta furaha ya uwepo wako katika maisha ya wale tunaotumikia.

### Ijumaa 12

Baba, tunaombea wale ambao wamezidiwa na kazi zao za kujitolea, ikiwa ni kutokana na hali ilio nje ya uwezo wao, au kutokana na wasiwasi wao. Wape nguvu mpya na kusudi la dhamira pale haya yote yanapohitajika; uwape ushauri wa busara na msaada wa vitendo pale ulio sahihi.

### Jumamosi 13

Bwana, tunatoa shukrani kwa ukarimu na ushirika wa zawadi zinazotolewa na wafanya kazi wa kujitolea katika jamii zetu. Mfano wao utuongoze kutoa kwa ukarimu zaidi kufikia wengine ambao wanahitaji msaada wetu.

### Wimbi la Maombi

**Juni 8-10:** **Yambio** Sudan Kusini; **Garissa**, Kenya; **Mbamili**, Nijeria; **Hereford** Uingereza; **Willockra**, Australia na **Thailand**

**Juni 11-13:** **Mahajanga**, Madagaska; **Mara**, Tanzania; **West Buganda**, Uganda; **Kwoi**, Nijeria; **Newcastle**, Australia; **East Kerala**, India

## Kumlaki Mgeni

14-20 Juni 2020

### Jumapili 14

Msisahau kuwakaribisha wageni; maana kwa kufanya hivyo watu wengine walipata kuwakaribisha malaika bila kujua. *Waebrania 13: 2*

### Jumatatu 15

'Wakati mimi nilihitaji jirani ulikuwepo?' Kuna majirani wengi amba wana mahitaji, hebu tukutane na kila mmoja wao kwa upendo wako kwa namna yeyote itakayowasaidia zaidi.

### Jumanne 16

'Nazo mila na rangi na jina hazitakuwa jambo la muhimu, mimi nitakuweko'. Tusaidie daima, Bwana, kuona watu wengine kama wewe uwaonao. Tusitoe hukumu kulingana na sura lakini tumtendee kila mtu kama yeye ni malaika wetu.

### Jumatano 17

'Nilikuwa na njaa na kiu; je ulikuwepo?' Tusaidie Bwana kuonyesha ukarimu wetu kwa watu wengine isipokuwa wale tunaowajua vizuri, na kukaribisha wale amba hatuwajui, ili tushiriki upendo wako kwa njia ya chakula na vinywaji kwa wote tunaokutana nao.

### Alhamisi 18

'Nilikuwa nasikia baridi, nilikuwa uchi, je ulikuweko?' Tunataka kutoa joto kwa wale wanaokabiliwa na baridi katika mwili, akili au nafsi, kisha tupambe kwa upendo wale amba ni wale mavu au masikini kwa sababu yoyote.

### Ijumaa 19

Tunaomba kwa ajili ya taabu zinazokabili wakimbizi na wale wasio na makazi, wale amba husafiri kwa kutafuta mahali tulivu. Bariki kazi ya wanachama wetu, amba hutoa misaada na kukaribisha watu kwa vitendo kwa jina la Kristo.

### Jumamosi 20

'Popote unaposafiri mimi nitakuwepo.' Tunaposafiri maishani, tunaomba Roho Mtakatifu atupatie maneno ya kusema na utambuzi wa kutenda ipasavyo. Tuweze kuwaona wale waliopotea, wale wanaona aibu na wale walio wapweke, na kama Yesu anavyofanya, tulete mwanga katika maisha yao.

## Wimbi la Maombi

**Juni 17:** **Bukavu** Kongo; **Nyahururu**, Kenya; **Gboko**, Nijeria; **Portsmouth**, Uingereza na **New Guinea Islands**, Papua New Guinea

**Juni 18-20:** **Rejaf**, Sudan Kusini; **Military Episcopate**, Kenya; **Doko & Owo**, Nijeria; **Chelmsford**, Uingereza na **Jamaika & Cayman Islands**

## Uzazi

21-27 Juni 2020

### Jumapili 21

Siku ya kina baba Oneni, basi, jinsi Baba alivyotupenda mno hata tunaitwa watoto wa Mungu! Na kweli, ndivyo tulivyo. Ndiyo maana ulimwengu haututambui sisi, kwani haumjui! *1 Yohana 3: 1*

### Jumatatu 22

Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa wazazi yetu waliotuzaa, kwa wazazi amba walitlea tukiwa watoto na kutusaidia kuwa watu tulio sasa. Tunaomba kwa ajili ya watoto wasio na wazazi na wale wanaoishi katika familia zinazoongozwa na watoto.

### Jumanne 23

Mungu Baba yetu, ulimtuma mwana wako katika ulimwengu wetu ili aishi mionganii mwetu. Tunawaombea wazazi ili waweze kujua kilicho bora kwa watoto wao, ili wawaongoze katika njia ikupendayo, na wapate ujasiri wa kuwaacha watoto wao watafute njia zao wakati wanaelekea kuwa watu wazima.

### Jumatano 24

Baba yetu uliye mbinguni, kama uliviyotazama mwana wako akiteseka na kufa kwa ajili yetu, tunakuomba uwe karibu na wazazi wale amba watoto wao wanaumbuliwa na ugonjwa au maradhi ya upunguvu.

### Alhamisi 25

Tunaombea ongezeko la ari za Ushirika wa Akina Mama kuhusu mipango ya uzazi duniani kote, ili familia kila mahali zipate furaha katika uzazi.

### Ijumaa 26

Tunaomba leo kwa ajili ya wote amba wangependa kuzaa watoto lakini hawawezi, kwa sababu yeyote ile, pia kwa wale amba wamepata watoto waliozaliwa wafu au watoto amba walifariki mara baadaß' ya kuzaliwa. Wapate moyo, upendo na huruma ya Kristo.

### Jumamosi 27

Tunawaombea wazazi amba wanajitahidi kukabiliana na maisha, amba maisha yao ya baadaye yako hatarini na kila kazi inaonekana kama mlima wa kupanda; wapate msaada na tegemeo wanazohitaji.

## Wimbi la Maombi

**Juni 22-24:** **Rumonge**, Burundi; **Tabora**, Tanzania; **Kabba & Bukuru**, Nijeria; **St Albans**, Uingereza na **Nagpur**, India

**Juni 25-27:** **Table Bay**, Afrika Kusini; **Rift Valley**, Tanzania; **Evo & Ijebu**, Nijeria; **Adelaide**, Australia na **Taejon**, Korea Kusini

**Jumapili 28**

Mwenyezi Mungu awaoneshe wema wake na kuwapa amani. *Hesabu 6:26*

**Jumatatu 29**

Mchungaji wetu mwenye upendo, tunakuangazia wewe kutuongoza na kutupumzisha katika malisho ya upendo wako. Maji ya amani yako yatuletee nguvu mpya katika roho zetu, tuweze kukabiliana na changamoto za maisha kwa roho tulivu. Huku tukipumzika mbele zako, Roho wako Mtakatifu apumue juu yetu na kutuliza mioyo yetu.

**Jumanne 30**

Bwana, tunaomba leo kwa ajili ya wote ambao wanakabiliwa na mizigo katika shughuli za maisha. Tunaomba kwamba upendo wa Kristo uguse mioyo yao na kuleta utulivu ndani ya licha ya changamoto zinazowakabili.

**Wimbi la Maombi**

**Juni 29-30: Zambia Mashariki, Zambia; Mombasa, Kenya; Gwagwalada & Ekiti-West, Nijeria; Leicester, Uingereza na Temotu, Visiwa vya Solomon**

**Ushirika wa Akina Mama**  
ni shirika la kimataifa la kujitolea, linaloongozwa na wanawake. Tukiwa na umoja katika tofauti zetu, tukiishi katika imani yetu, sisi hutoa msaada kwa watu binafsi na familia ili maisha yao yabadilike. Tukiwa ndani ya Kanisa na jamii, tunafikia watu kwa njia maalum na kuwapatia sauti wale walioshutumiwa na wale wanaoishi katika mazingira magumu duniani kote.



Christian care for families

# Duka la Ushirika wa Akina Mama Katika Mtandao

Uchaguzi mpana wa bidhaa zenyenye nembo ya  
Ushirika wa Akina Mama, beji, machapisho na zaidi!

[www.mueshop.org](http://www.mueshop.org)



Tunawasilisha kote duniani